KATIBA YA CCM:Layout 1 6/5/10 11:58 AM Page 1

# KATIBA YA CHAMA CHA MAPINDUZI 1977

TOLEO LA 2010

BEI SH.500/-

KATIBA YA CCM:Layout 1  6/5/10  11:58 AM  Page 3

# KATIBA
# YA
# CHAMA CHA MAPINDUZI

## 1977

**TOLEO LA 2010**

*Toleo hili la Katiba ya Chama Cha Mapinduzi la 2010 ni Toleo la Kumi na Nne tangu Katiba hii itungwe kwa mara ya kwanza mwaka 1977.*

*Kwa hali hii ni Toleo ambalo limezingatia na kuweka pamoja marekebisho yaliyofanywa katika Katiba ya Chama Cha Mapinduzi ya 1977 matoleo ya 1980, 1982, 1984, 1987, 1990, Machi 1992, Septemba1992, 1994, 1995, 1997 , 2005 na 2007.*

## YALIYOMO

Uk.

1. Azimio la Mkutano Mkuu wa Taifa wa pamoja wa TANU na ASP ........................1

2. **SEHEMU YA KWANZA:-**
   Jina, Imani na Madhumuni .......................5

3. **SEHEMU YA PILI:-**
   Wanachama na Uongozi..........................11

4. **SEHEMU YA TATU:-**
   (i) Vikao vya Shina ..............................21
   (ii) Vikao vya Tawi ................................29
   (iii) Vikao vya Kata/Wadi .......................51
   (iv) Vikao vya Jimbo .............................73
   (v) Vikao vya Wilaya.............................93
   (vi) Vikao vya Mkoa...............................121
   (vii) Vikao vya Taifa .............................149

5. **SEHEMU YA NNE:-**
   Wazee na Jumuiya za Wananchi ..........195

6. **SEHEMU YA TANO:-**
   Mengineyo .........................................197

7. Ahadi za Wanachama wa Chama cha Mapinduzi .........................201

8. Katiba, Kanuni na Taratibu za Utekelezaji ......................................202

KATIBA YA CCM:Layout 1 6/5/10 11:58 AM Page 8

# KATIBA YA CHAMA CHA MAPINDUZI

## AZIMIO LA MKUTANO MKUU WA TAIFA WA PAMOJA WA TANU NA ASP

Kwa kuwa Mkutano Mkuu wa Taifa wa pamoja, kwa niaba ya Wana-TANU na Wana-ASP, kwa pamoja unaelewa na kukubali kwamba jukumu letu katika Historia ya Taifa ni kuimarisha Umoja, kuleta Mapinduzi ya Kijamaa Tanzania na kuendeleza mapambano ya Ukombozi katika Afrika na kote duniani;

Kwa kuwa tunatambua kuwa Mapambano ya Kujenga Ujamaa katika Tanzania na kushiriki kwetu kwa ukamilifu katika harakati za Mapinduzi ya Afrika na Dunia kunahitaji Chombo madhubuti cha uongozi kinachounganisha fikira na vitendo vya wafanyakazi na wakulima;

Kwa kuwa tunazingatia na kuthamini kazi nzuri ya kimapinduzi na ya mafanikio makubwa iliyokwishafanywa na TANU na ASP katika kumwondoa Mwafrika kutoka kwenye unyonge wa kunyonywa, kunyanyaswa na kudharauliwa na kumfikisha kwenye uhuru na kuheshimiwa;

Kwa kuwa tunatambua kuwa Umoja wa TANU na ASP unatokana na ushirikiano wetu wa miaka mingi tangu wakati wa Mapambano ya kupigania Uhuru hadi sasa, na unatokana pia na Siasa yetu moja ya Ujamaa na Kujitegemea;

Kwa kuwa tunatambua pia kwamba kuweko kwa Vyama viwili katika mazingira ya Chama kimoja cha Siasa kunapunguza upeo wa Nguvu na Umoja wetu katika kuendeleza mapambano ya kujenga ujamaa nchini na kushiriki kwa pamoja kwa ukamilifu katika harakati za mapinduzi ya Tanzania, ya Afrika na ya dunia;

Kwa kuwa, kihistoria, tumeongozwa na kumbukumbu ya kitendo kama hiki cha kimapinduzi na busara ambacho Waanzilishi wa TANU, chini ya Uongozi wa Mwalimu Julius K. Nyerere walikifanya hapo awali cha kuvunja Chama cha African Association na kuunda TANU, na waanzilishi wa ASP chini ya uongozi wa Marehemu Abeid Amani Karume, walikifanya hapo awali cha kuvunja Vyama vya African Association na Shiraz Association na kuunda ASP, shabaha yao wote ikiwa ni kuunda Chama kipya madhubuti na cha kimapinduzi chenye uwezo mkubwa zaidi wa kuongoza mapambano ya wananchi wetu katika mazingira mapya ya wakati huo.

Kwa hiyo basi:-

(1) Sisi wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa pamoja wa TANU na ASP tuliokutana leo tarehe 21 Januari, 1977 mjini Dar es Salaam, chini ya uongozi wa pamoja wa Mwalimu Julius K. Nyerere Rais wa TANU na Ndugu Aboud Jumbe, Rais wa ASP, kwa kauli moja tunaamua na kutamka rasmi kuvunjwa kwa TanganyikaAfrican National Union (TANU) na

Afro Shirazi Party (ASP) ifikapo tarehe 5 Februari, 1977, na wakati huo huo kuundwa kwa Chama kipya cha pekee na chenye uwezo wa mwisho katika mambo yote kwa mujibu wa Katiba.

(2) Vyama vya TANU na ASP vinavunjwa kwa taadhima kubwa. TANU na ASP havikuamua kujivunja kama vyama kwa kuwa vimeshindwa kutekeleza jukumu lao. Kwa hakika TANU na ASP ni Vyama vilivyopata mafanikio ya kipekee katika Afrika katika kulitekeleza jukumu la kihistoria na mafanikio hayo ndiyo leo yamewezesha kitendo hiki cha Vyama viwili kujivunja vyenyewe. TANU na ASP vitaheshimiwa siku zote kama viungo muhimu katika Historia ya Mapambano ya Ukombozi wa Taifa letu na wa Bara la Afrika, na waanzilishi wa TANU na ASP watakumbukwa daima kama mashujaa wa taifa letu waliotuwezesha leo kupiga hatua hii ya kufungua ukurasa mpya katika Historia ya Tanzania.

(3) Tumeamua kwa pamoja kuunda Chama kipya cha kuendeleza mapinduzi ya kijamaa nchini Tanzania na Mapambano ya Ukombozi wa Afrika juu ya misingi iliyojengwa na TANU na ASP.

Chama tunachokiunda tunataka kiwe chombo madhubuti katika muundo wake na hasa katika fikra

zake na vitendo vyake vya kimapinduzi vya kufutilia mbali aina zote za unyonyaji nchini, na kupambana na jaribio lolote lile la mtu kumuonea mtu au shirika au chombo cha nchi kuonea na kudhalilisha wananchi, kudhoofisha uchumi au kuzorotesha maendeleo ya Taifa;

Chama tunachokiunda tunataka kishike barabara hatamu za uongozi wa shughuli zote za umma kwa maslahi ya Wafanyakazi na Wakulima wa Taifa letu;

Chama tunachokiunda tunataka kiwe kiungo kati ya Wanamapinduzi wa Tanzania na Wanamapinduzi wenzetu kokote waliko.

## SEHEMU YA KWANZA

## JINA, IMANI NA MADHUMUNI

1. Jina la Chama litakuwa CHAMA CHA MAPINDUZI, kwa kifupi CCM. *Jina la Chama*

2. Makao Makuu ya CCM yatakuwa Dodoma na kutakuwa na Afisi Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Zanzibar na Ofisi Ndogo ya Makao Makuu Dar es Salaam. *Makao Makuu ya Chama*

3. Bendera ya CCM itakuwa na rangi ya kijani kibichi, ambayo itakuwa na alama ya Jembe (alama ya mkulima) na Nyundo (alama ya mfanyakazi) kwenye pembe ya juu upande wa mlingoti. *Bendera ya CCM*

4. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba: *Imani ya CCM*
   (1) Binadamu wote ni sawa.

   (2) Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

   (3) Ujamaa na Kujitegemea ndiyo njia pekee ya kujenga jamii ya watu walio sawa na huru.

5. Kwa hiyo Malengo na Madhumuni ya CCM yatakuwa yafuatayo:- *Malengo na Madhumuni ya CCM*
   (1) Kushinda katika Uchaguzi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa Tanzania Bara

na Zanzibar ili kuunda na kushika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande mmoja na Zanzibar kwa upande wa pili.

(2) Kulinda na kudumisha Uhuru wa Nchi yetu na raia wake.

(3) Kuhimiza ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea kwa mujibu wa Azimio la Arusha.

(4) Kusimamia utekelezaji wa Siasa ya CCM pamoja na kuendeleza fikra za viongozi waasisi wa vyama vya TANU na ASP, kama zilivyofafanuliwa katika maandiko mbali mbali ya Vyama hivyo
.

(5) Kuona kwamba kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika Jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake kwa mujibu wa sheria.

(6) Kuona kwamba katika Nchi yetu kila mtu aliye na uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi; na kazi maana yake ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu riziki yake.

(7) Kusimamia haki na maendeleo ya Wakulima, Wafanyakazi na wananchi

wengine wenye shughuli halali za kujitegemea; na hasa kuona kwamba kila mtu ana haki ya kupata malipo yanayostahili kutokana na kazi yake.

(8) Kuona kwamba kwa kutumia Vikao vilivyowekwa, raia anayo haki ya kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi wa mambo ya Taifa na yanayomhusu, na kwamba anao uhuru wa kutoa mawazo yake, wa kwenda anakotaka, wa kuamini Dini anayotaka na kukutana na watu wengine,maadamu havunji Sheria au Taratibu zilizowekwa.

(9) Kuona kwamba Nchi yetu inatawaliwa kwa misingi ya kidemokrasia na ya kijamaa.

(10) Kuhifadhi, kukuza na kudumisha imani na moyo wa kimapinduzi miongoni mwa Watanzania pamoja na ushirikiano na wanamapinduzi wenzetu kokote waliko.

(11) Kuweka na kudumisha heshima ya binadamu kwa kufuata barabara Kanuni za Tangazo la Dunia la Haki za Binadamu.

(12) Kuona kwamba Dola inakuwa Mhimili wa Uchumi wa Taifa.

(13) Kuona kwamba Serikali na Vyombo vyote vya Umma vinasaidia kwa vitendo kuanzishwa na kuendeleza shughuli za Ushirika na za ujamaa, na shughuli nyinginezo halali za wananchi za kujitegemea.

(14) Kuona kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya Wananchi na hasa jitihada za kuondosha umasikini, Ujinga na Maradhi.

(15) Kuona kwamba Serikali na vyombo vyote vya umma vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wanawake na wanaume bila kujali rangi, kabila, Dini, au hali ya mtu.

(16) Kuona kwamba katika nchi yetu hakuna aina yoyote ya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu na/au upendeleo.

(17) Kuendelea kupiga vita Ukoloni Mamboleo, Ubeberu na Ubaguzi wa aina yoyote.

(18) Kuimarisha uhusiano mwema na Vyama vyote vya Siasa vya Nchi nyingine vyenye itikadi kama ya CCM ambavyo kweli vinapinga Ukoloni,

Ukoloni Mamboleo, Ubeberu na Ubaguzi wa aina yoyote.

(19) Kushirikiana na Vyama vingine katika Afrika, kwa madhumuni ya kuleta Umoja wa Afrika, na kuona kwamba Serikali inaendeleza na kuimarisha ujirani mwema.

5 A. Katika katiba hii, maneno yafuatayo yatakuwa na maana inayoonyeshwa kwa kila neno linalohusika: Ufafanuzi

'Wabunge wa aina nyingine' maana yake ni Wabunge wa Viti Maalum, Wabunge wa kuteuliwa pamoja na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, wanaotokana na CCM.

'Wawakilishi' maana yake ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wanaotokana na CCM.

'Kanuni zinazohusika' maana yake ni Kanuni za CCM zinazohusika, zilizoorodheshwa katika Nyongeza 'B' ya Katiba hii.

Kwa ajili ya kuondoa utata unaoweza kujitokeza, inafafanuliwa zaidi kwamba endapo Kanuni yoyote itaonekana kuwa inapingana na Masharti ya Katiba hii, masharti ya Katiba ndiyo yatakayofuatwa.

## SEHEMU YA PILI

## WANACHAMA NA VIONGOZI

### FUNGU LA 1:

### WANACHAMA

6. Kila mtu aliyekuwa mwanachama wa TANU au wa ASP mara kabla ya kuvunjwa kwa Vyama hivyo, na aliyekuwa anatimiza masharti ya Uanachama wake, atakuwa mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi, isipokuwa kama atakataa mwenyewe. *Wanachama Waasisi*

7. Raia yeyote wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18, anaweza kuwa Mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi iwapo anakubali Imani, Malengo na Madhumuni ya CCM. *Wanachama Wapya*

8. Mtu atakayekubaliwa kuingia katika CCM, au kuendelea kuwa Mwanachama, ni yule anayetimiza Masharti yafuatayo:- *Masharti ya Uanachama*

   (1) Kuwa mtu anayeheshimu watu.

   (2) Kuwa mtu anayefanya juhudi ya kuielewa, kuieleza, kuitetea na kuitekeleza Itikadi na Siasa ya CCM.

(3) Kuwa mtu mwenye kuamini kuwa kazi ni kipimo cha Utu, na kuitekeleza imani hiyo kwa vitendo.

(4) Kuwa mtu anayependa kushirikiana na wenzake.

(5) Kuwa mtu ambaye siku zote yuko mstari wa mbele katika utekelezaji wa mambo yote ya Umma, kulingana na Miongozo ya CCM.

(6) Kuwa wakati wote ni mfano wa tabia nzuri kwa vitendo vyake na kauli yake, kuwa mwaminifu na kutokuwa mlevi au mzururaji.

(7) Kuwa ama Mkulima, Mfanyakazi, au mwenye shughuli nyingine yoyote halali ya kujitegemea.

Utaratibu wa kuomba Uanachama

9. Mtu atakayetaka kuwa Mwanachama atajaza fomu ya maombi na kuipeleka kwa Katibu wa Tawi anapoishi.

Utaratibu wa kufikiria maombi ya Uanachama

10. Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itafikiria na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu maombi ya Uanachama.

Mafunzo kwa Wanachama

11. CCM itakuwa na Mpango wa kutoa Mafunzo kwa wanachama wake juu ya Imani, Malengo na Madhumuni ya Siasa ya CCM kwa jumla.

12. (1) Mtu akikubali kuwa Mwanachama itabidi atekeleze haya yafuatayo:- *Kiingilio na Ada za Uanachama*

(a) Atatoa kiingilio cha Uanachama.

(b) Atalipa ada ya Uanachama kila mwezi isipokuwa kama akipenda anaweza kulipa ada ya mwaka mzima mara moja.

(c) Atatoa michango yoyote itakayoamuliwa.

(2) Viwango vya kiingilio, ada na michango vitawekwa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

13. (1) Uanachama wa mwanachama utakwisha kwa:- *Kuondoka katika Chama*

(a) Kufariki.

(b) Kujiuzulu mwenyewe.

(c) Kuachishwa kwa mujibu wa Katiba.

(d) Kufukuzwa kwa mujibu wa Katiba.

(e) Kutotimiza masharti ya uanachama.

(f) Kujiunga na Chama kingine chochote cha siasa.

(2) Mwanachama ambaye uanachama wake unakwisha kwa sababu yoyote ile hatarudishiwa kiingilio alichokitoa, ada aliyotoa wala michango yoyote aliyoitoa.

(3) Mwanachama aliyeachishwa au kufukuzwa Uanachama akitaka kuingia tena katika CCM, itabidi aombe upya, na atapeleka maombi yake hayo ama katika Halmashauri Kuu ya Wilaya ama kikao kilichomwachisha au kumfukuza Uanachama.

(4) Mwanachama aliyejiuzulu akitaka kuingia tena katika CCM ataomba upya kwa kufuata utaratibu wa kuomba Uanachama kwa mujibu wa Katiba ya CCM.

Haki za Mwanachama

14. Mwanachama yeyote atakuwa na haki zifuatazo:-

(1) Haki ya kushiriki katika shughuli zote za CCM kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

(2) Haki ya kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya CCM pale ambapo anahusika kwa mujibu wa Katiba.

(3) Haki ya kuomba kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa CCM na ya kuchagua viongozi wake wa CCM kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Taratibu za CCM.

(4) Haki ya kujitetea au kutoa maelezo yake mbele ya Kikao cha CCM

kinachohusika katika mashtaka yoyote yaliyotolewa juu yake, pamoja na haki ya kukata rufani ya kwenda katika Kikao cha juu zaidi cha CCM kama kipo endapo hakuridhika na hukumu iliyotolewa.

(5) Haki ya kumuona kiongozi yeyote wa CCM maadam awe amefuata utaratibu uliowekwa.

(6) Haki ya kupiga Kura yake ya Maoni kwa wagombea wa CCM wa nafasi za Udiwani wa Kata/Wadi, Ubunge na Uwakilishi wa Jimbo kwa kufuata masharti ya Kanuni za CCM.

15. Kila Mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao:- Wajibu wa Mwanachama

(1) Kujua kwamba Chama Cha Mapinduzi ndicho chenye nguvu, uwezo na kwamba nguvu hizo zinatokana na umoja wa Wanachama, fikira sahihi za CCM na kukubalika kwake na umma. Kwa hiyo kulinda na kuendeleza mambo hayo ni Wajibu wa kwanza wa kila Mwanachama.

(2) Kutumikia nchi yake na watu wake wote kwa kutekeleza wajibu wake bila hofu, chuki wala upendeleo wa nafsi yake, rafiki au jamaa.

(3) Kujitolea nafsi yake kuondosha Umasikini, Ujinga, Maradhi na Dhuluma, na kwa jumla kushirikiana na wenzake wote katika kujenga Nchi yetu.

(4) Kuwa wakati wote mkweli, mwaminifu na raia mwema wa Tanzania.

(5) Kukiri kwa imani na kutekeleza kwa vitendo Siasa ya CCM ya Ujamaa na Kujitegemea.

(6) Kujielimisha kwa kadiri ya uwezo wake, na kutumia elimu hiyo kwa faida ya wote.

(7) Kuwa tayari kujikosoa na kukosolewa ili kuweza kuwa na msimamo sahihi wa siasa ya CCM.

(8) Kuwa wakati wowote hadaiwi ada zozote za Uanachama.

(9) Kuhudhuria mikutano ya CCM inayomhusu.

## FUNGU LA II

## VIONGOZI

16. Kiongozi wa CCM ni kila Mwanachama mwenye dhamana yoyote katika CCM aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba. Maana ya Kiongozi

17. Pamoja na kutimiza masharti ya Uanachama kama yalivyoelezwa katika Katiba, Kiongozi sharti pia awe na sifa zifuatazo:- Sifa za Kiongozi

    (1) Awe ni mtu aliyetosheka na asiwe mtu aliyetawaliwa na tamaa.

    (2) Awe ni mtu anayependa kueneza matunda ya Uhuru kwa wananchi wote kwa ajili ya manufaa yao na maendeleo ya Taifa kwa jumla.

    (3) Awe na sifa nyingine kama zilivyowekwa katika Kanuni zinazohusika.

18. Ni mwiko kwa kiongozi:- Miiko ya Kiongozi

    (1) Kutumia madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo, au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo.

(2) Kupokea mapato ya kificho, kutoa au kupokea rushwa, kushiriki katika mambo yoyote ya magendo au mambo mengine yaliyo kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo.

(3) Miiko mingine ya Viongozi itakuwa kama ilivyowekwa katika Kanuni zinazohusika.

Kuondoka katika uongozi

19. (1) Uongozi wa kiongozi utakoma kwa:-

(a) Kufariki

(b) Kujiuzulu mwenyewe.

(c) Kuachishwa kwa mujibu wa Katiba.

(d) Kufukuzwa kwa mujibu wa Katiba.

(e) Kung'atuka /kuacha kazi.

(f) Kujiunga na chama kingine chochote cha siasa.

(2) Kiongozi aliyeachishwa au kufukuzwa uongozi anaweza kuomba tena nafasi ya uongozi wowote na maombi yake yatafikiriwa na kutolewa uamuzi na kikao kilichomwachisha au kumfukuza uongozi.

20. (1) Mwanachama anayeomba nafasi ya uongozi wa aina yoyote katika CCM hatakubaliwa kuwa amechaguliwa mpaka awe amepata zaidi ya nusu ya kura halali zilizopigwa.

Kiwango cha kura katika uchaguzi wa Viongozi

(2) Katika uchaguzi wa kujaza nafasi nyingi kwa pamoja, ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura alizopata mwombaji wa nafasi hiyo zaidi ya wenzake, bila kujali kama kura hizo zinafikia nusu ya kura halali zilizopigwa.

(3) Kanuni za Uchaguzi wa CCM zitaweka vifungu mahsusi, vitakavyowezesha uwakilishi wa Wanawake katika vikao vya CCM hatimaye kuwa si chini ya asilimia 50 ya wajumbe wote wanaochaguliwa kujaza nafasi za makundi, kwa kila ngazi ya uongozi wa Chama.

KATIBA YA CCM:Layout 1 6/5/10 11:58 AM Page 28

## SEHEMU YA TATU

## VIKAO VYA CCM

## FUNGU LA 1:

## VIKAO VYA SHINA

21. Kikao cha mwanzo kabisa cha CCM kitakuwa ni kikao cha Shina. Hapa ndipo kila mwanachama atadhihirisha uanachama wake kwa kutekeleza kwa vitendo wajibu wake wa uanachama. Aidha hapa ndipo alama zinazokitambulisha Chama kama vile bendera, zitakapoanzia kutumika. Shina

22. (1) Kutakuwa na aina zifuatazo za Mashina:- Aina za Mashina

(i) Mashina ya Ndani ya Nchi:-

(a) Mashina yaliyoundwa katika maeneo ya makazi katika nyumba kumi zilizohesabiwa na kuwekwa pamoja kwa madhumuni ya kuunda shina.

(b) Mashina maalum yaliyoundwa katika Ofisi za CCM, Jumuiya za Wanainchi zinazoongozwa na CCM na Taasisi nyingine za CCM.

(c) Mashina ya Wakereketwa /Maskani yaliyoundwa na wanachama wa CCM katika maeneo husika, baada ya kupata idhini ya Kamati ya Siasa ya Wilaya.

(ii) Mashina ya Nje ya Nchi:-
Mashina yaliyoundwa Nje ya Nchi katika maeneo wanakoishi wanachama wa CCM, baada ya kupata idhini ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(2) Ili Wanachama waweze kuunda Shina, idadi yao isiwe chini ya watano.

(3) Kila Shina la eneo la makazi au lililo nje ya nchi na kila Shina Maalum litachagua Kiongozi wa Shina kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa ambaye atajulikana kama Balozi wa Shina. Aidha kila Shina la Wakereketwa/Maskani litachagua Kiongozi wa Shina kwa utaratibu uliowekwa ambaye atajulikana kama Mwenyekiti wa Shina la Wakereketwa au la Maskani.

(4) Kila Shina lenye Wanachama wasiopungua kumi (10) litachagua Kamati itakayoitwa Kamati ya Uongozi ya Shina yenye wajumbe watano

akiwemo Balozi/Mwenyekiti wa Shina hilo. Katibu wa Shina atachaguliwa na Kamati ya Uongozi ya Shina.

23. Pamoja na wajibu mwingine wowote unaowahusu wanachama kwa jumla, kila Shina litakuwa na wajibu ufuatao:- Wajibu wa Shina

(1) Kulinda na kuendeleza Siasa ya CCM katika Shina.

(2) Kuona kwamba unakuwepo ulinzi na usalama wa umma katika eneo lake.

(3). Kueneza itikadi na Siasa ya CCM katika Shina.

(4) Kutekeleza ipasavyo maamuzi na maagizo ya ngazi za juu ya CCM na ya Serikali pamoja na shughuli nyinginezo za umma.

24. Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya CCM katika kila Shina:- Vikao vya CCM vya Shina

(1) Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina.

(2) Mkutano wa Wanachama wote wa Shina.

(3) Kamati ya Uongozi ya Shina pale panapohusika.

25. (1) Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina utakuwa na wajumbe wafuatao:- Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina

(a) Balozi/Mwenyekiti wa Shina

(b) Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Shina pale panapohusika kwa mujibu wa Katiba.

(c) Wanachama wengine wote wa Shina hilo.

(2) Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina ndicho kikao kikuu cha CCM katika Shina.

(3) Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina utafanyika kwa kawaida mara moja kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo, au kwa maagizo ya vikao vya juu.

(4) Balozi/Mwenyekiti wa Shina ataongoza Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina. Lakini Balozi/Mwenyekiti wa Shina asipoweza kuhudhuria, Mkutano unaweza kumchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina

26. Kazi za Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kufikiria taarifa ya kazi za CCM katika Shina na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu maendeleo kwa jumla katika Shina.

(3) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.

(4) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Balozi/Mwenyekiti wa Shina.

(b) Kuwachagua wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Shina pale panapohusika.

27. (1) Kutakuwa na Mkutano wa Wanachama wote wa Shina kwa kila Shina. Mkutano wa Wanachama wote wa Shina

(2) Mkutano wa wanachama wote wa Shina utazungumzia mambo yenye maslahi ya CCM na ya wananchi mahali pale Shina lilipo, kama vile shughuli za Ulinzi na Usalama, maendeleo katika Shina na kufikisha mapendekezo ya wanachama katika vikao vya juu.

(3) Utawapigia kura za maoni wana-CCM wanaogombea nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji/Mtaa wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(4) Mkutano wa Wanachama wote utafanyika kwa kawaida si chini ya mara moja kwa mwezi.

(5) Kiwango cha mahudhurio katika mikutano ya wanachama wote katika Shina kitakuwa ni zaidi ya theluthi moja ya wajumbe walio na haki ya kuhudhuria kikao hicho.

(6) Balozi/Mwenyekiti wa Shina ataongoza Mkutano wa wanachama wote wa Shina lakini asipoweza kuhudhuria, Mkutano utamchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kamati ya Uongozi ya Shina

28. Kamati ya Uongozi ya Shina pale panapohusika kwa mujibu wa Katiba itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(1) Balozi/Mwenyekiti wa Shina

(2) Wajumbe wanne wa Kamati ya Uongozi ya Shina.

Kazi za Kamati ya Uongozi ya Shina

29. Kazi za Kamati ya Uongozi ya Shina zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yote ya CCM na utendaji kazi katika Shina.

(2) Kuandaa shughuli za vikao vyote vya CCM vya Shina.

30. (1) Balozi/Mwenyekiti wa Shina atachaguliwa na Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina. Balozi wa Shina
Atakuwa katika nafasi ya Uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(2) Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo ya CCM na utendaji kazi katika Shina.

(3) Atakuwa kiungo cha wanachama wote katika Shina.

(4) Atakuwa ndiye mwenezi na mhamasishaji mkuu wa Siasa ya CCM katika eneo lake.

(5) Atakuwa na wajibu wa kuwaeleza Wanachama maamuzi yote ya CCM, kuwaongoza na kuwashirikisha katika utekelezaji wa maamuzi hayo, na kufikisha mapendekezo ya wanachama katika vikao vya juu.

(6) Atakuwa na wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa mambo yote ya siasa katika Shina lake.

(7) Atakuwa na wajibu wa kujenga uhusiano mwema wa wakazi wa Shina lake kwa lengo la kuunda mazingira ya amani na utulivu.

(8) Ataongoza Kamati ya Uongozi ya Shina pale panapohusika.

(9) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Mwaka wa CCM wa Shina, na Mkutano wa Wanachama wote wa Shina.

(10) Katika Mikutano anayoongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, atakuwa pia na kura ya uamuzi, endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana.

Isipokuwa kwamba kama Kikao anachokiongoza ni Kikao cha Uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za Wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

## FUNGU LA II

## VIKAO VYA TAWI

31. (1) Kutakuwa na aina nne za Matawi ya CCM kama ifuatavyo:- Aina za Matawi ya CCM

(a) Matawi ambayo yameundwa vijijini ambayo yataitwa Matawi ya Vijijini.

(b) Matawi ambayo yameundwa katika maeneo wanayoishi watu mijini ambayo yataitwa Matawi ya Mitaani.

(c) Matawi maalum ambayo yameundwa kwenye Ofisi za CCM, Taasisi za CCM, na Taasisi nyingine zinazoongozwa na CCM.

(d) Matawi ambayo yameundwa nje ya nchi yenye wanachama wa CCM wengi wanaoishi katika sehemu mbalimbali za nchi hiyo na ambao wana Mashina yao. Matawi haya yatafunguliwa kwa idhini ya Kamati Kuu.

(2) Tawi litafunguliwa tu iwapo mahali hapo panapohusika kuna Wanachama wasiopungua hamsini na wasiozidi mia sita.

Vikao vya CCM vya Tawi

32. Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya CCM katika kila Tawi:-

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi.

(2) Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(4) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(5) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi

33. (1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi utakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(b) Katibu wa CCM wa Tawi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

(e) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(f) Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Mtaa/Kitongoji anayetokana na CCM, anayeishi katika Tawi hilo.

(g) Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi waliomo katika Tawi hilo.

(h) Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya waliomo katika Tawi hilo.

(i) Mabalozi wa Mashina wa Tawi hilo.

(j) Wenyeviti wa Mashina ya Wakereketwa/ Maskani ya Tawi hilo.

(k) Mwenyekiti na Katibu wa Tawi wa Jumuiya inayoongozwa au iliyo jishirikisha na CCM, na Mjumbe mmoja mwingine ambaye ni Mwanachama wa CCM aliyechaguli wa na kila Jumuiya iliyomo katika Tawi hilo.

(l) Diwani anayetokana na CCM anayeishi katika Tawi hilo.

(m) Wanachama wengine wote wa Tawi hilo.

(2) Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi ndicho kikao kikuu cha CCM katika Tawi.

(3) Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi utafanyika kwa kawaida mara moja kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya kikao cha juu.

(4) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi ataongoza Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Mkutano huo unaweza kumchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi

34. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kupokea na kujadili Taarifa ya Kazi za CCM katika Tawi, iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.

(3) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu Ulinzi na Usalama na Maendeleo kwa jumla katika Tawi hilo.

(4) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi

utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(b) Kuwachagua wajumbe watano wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi.

(c) Kumchagua mjumbe mmoja wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo na wa Wilaya.

(d) Kuwachagua wajumbe kumi wa kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(5) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

35. (1) Kutakuwa na Mkutano wa Wanachama wote wa CCM katika kila Tawi. Mkutano wa wanachama wote wa Tawi

(2) Mkutano huo utazungumzia mambo yaliyo na maslahi ya CCM na ya wananchi mahali pale Tawi lilipo, kama vile shughuli za Ulinzi na Usalama, na maendeleo katika Tawi.

(3) Mkutano wa Wanachama wote utafanyika kwa kawaida mara moja katika kila miezi mitatu, lakini unaweza

kufanyika wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya kikao cha juu.

(4) Kiwango cha mahudhurio katika Mikutano ya Wanachama wote katika Tawi kitakuwa zaidi ya theluthi moja ya Wajumbe wake wenye haki ya kuhudhuria kikao hicho.

(5) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi ataongoza Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi, lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Mkutano utamchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

(6) Siku ya kupiga Kura za maoni kwa wagombea wa ngazi za Kijiji na Mtaa, wana CCM wote watapiga Kura zao za maoni wakiwa katimka Matawi ya Vijijini au Mitaani ambako wanaishi na ambako wao ni wanachama.

Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

36. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(b) Katibu wa CCM wa Tawi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

(e) Wajumbe kumi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi.

(f) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi hilo.

(g) Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Mtaaanayetokana na CCM anayeishi katika Tawi hilo.

(h) Mjumbe mmoja wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi hilo.

(i) Mwenyekiti na Katibu wa Tawi wa Jumuiya inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM, na Mjumbe mmoja mwingine ambaye ni Mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya inayohusika iliyomo katika Tawi hilo.

(j) Wenyeviti wa Vitongoji wanaotokana na CCM wanaoishi katika Tawi hilo.

(k) Diwani anayetokana na CCM anayeishi katika Tawi hilo.

(l) Mabalozi/Wenyeviti wote wa Mashina katika Tawi hilo.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itafanya Mikutano yake ya kawaida mara moja kila miezi mitatu lakini inaweza kufanya Mkutano usiokuwa wa kawaida wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi ataongoza Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi;. lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Tawi atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

37. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya kila Tawi zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia Ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea katika eneo la Tawi.

(2) Kueneza Siasa na kueleza mipango ya CCM kwa Wanachama wote wa Tawi na kutafuta kila njia inayofaa ya kuimarisha CCM katika eneo la Tawi.

(3) Kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kufanya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Tawi.

(4) Kuona kwamba unakuwepo Ulinzi na Usalama katika eneo la Tawi.

(5) Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama na viongozi wa CCM katika Tawi, na inapolazimu kutoa taarifa kwa vikao vya CCM vinavyohusika.

(6) Kuongoza Mashina ya Tawi hilo katika vitendo na njia zinazofaa za kuimarisha CCM.

(7) Kufikisha maazimio na maagizo ya Vikao vya CCM vya juu kwa Wanachama, na kufikisha mapendekezo ya Wanachama katika vikao vya juu.

(8) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kufikiria na kufanya Uteuzi wa Mwisho wa wanachama wanaoomba nafasi za uongozi wa Shina la CCM na za uongozi wa Shina la UVCCM.

(b) Kumchagua Katibu wa CCM wa Tawi;

(c) Kumchagua Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(d) Kumchagua Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

(e) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi juu ya Wanachama wa CCM wanoomba kugombea Uenyekiti wa Vitongoji kwa mujibu wa Sheria za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(f) Kuwachagua wajumbe watano wa kuingia katika Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi kutoka miongoni mwao.

(9) Kujaza nafasi wazi za uongozi zinazotokea katika Tawi isipokuwa nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(10) Kuunda Kamati Ndogo za Utekelezaji kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa Siasa na kazi za CCM katika Tawi.

(11) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Ndogo za utekelezaji wa kazi za CCM katika Tawi.

(12) Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya CCM vilivyo chini yake.

(13) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM ya Tawi.

Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

38. (1) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(b) Katibu wa CCM wa Tawi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

(e) Wajumbe watano waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi kutoka miongoni mwao.

(f) Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Mtaa anayetokana na CCM anayeishi katika Tawi hilo.

(g) Diwani anayetokana na CCM anayeishi katika Tawi hilo.

(h) Mwenyekiti wa Tawi wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM iliyomo katika Tawi hilo.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itakutana si chini ya mara moja kila mwezi.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi ataongoza Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Tawi atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

39. Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika eneo lake.

(2) Kueneza itikadi na Siasa ya CCM katika Tawi.

(3) Kuandaa mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Tawi.

(4) Kusimamia Utekelezaji wa kila siku wa Siasa na maamuzi ya CCM chini ya Uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(5) Kupanga mipango ya kukipatia Chama mapato, kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mipango hiyo, kudhibiti mapato na kusimamia matumizi bora ya fedha na mali za Chama katika Tawi.

(6) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi juu ya wanachama wanaoomba kugombea nafasi za uongozi wa Tawi hilo; na uongozi wa jumuiya za CCM kupitia Tawi hilo.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi juu ya Wanachama wanaoomba nafasi ya uongozi wa Shina la CCM na UVCCM katika Tawi hilo.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi juu ya wanachama wa CCM wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa Kitongoji wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(d) Kufikiria na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi juu ya Wanachama wanaoomba nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi, Udiwani, Uenyekiti wa Mtaa, Ujumbe wa Kamati ya Mtaa, Uenyekiti wa Kijiji na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia Tawi hilo kwa mujibu wa sheria za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(e) Inapofika siku ya kupiga kura za maoni kwa waombaji wa nafasi za Udiwani, Ubunge na Uwakilishi:
Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Tawi itakuwa na wajibu wa kuhakiki uhalali wa uanachama wa CCM kwa kila mwanachama wa CCM wa Tawi lake anayefika katika kituo cha kupigia kura za maoni kilichowekwa katika Tawi hilo ili mwanachama huyo aweze kuruhusiwa kupiga kura za maoni

(7) Kufikiria na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu maombi ya Uanachama.

(8) Kuandaa mikutano ya Halmashauri kuu ya CCM katika Tawi

(9) Kuona kwamba unakuwepo Ulinzi na Usalama wa umma katika Tawi.

40. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao: Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

(a) Katibu wa CCM wa Tawi ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

(d) Makatibu wa Matawi ya Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM.

41. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Tawi yatakuwa yafuatayo:- Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi

(a) Kuongoza na kusimamia shughuli za Chama katika Tawi.

(b) Kuandaa Vikao vyote vya CCM katika Tawi.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Tawi yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu wa CCM wa Tawi.

(b) Idara ya Siasa na Uenezi ya Tawi.

(c) Idara ya Uchumi na Fedha ya Tawi.

(d) Idara ya Organaizesheni ya Tawi.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Tawi isipokuwa kwamba Katibu wa CCM wa Tawi atakuwa ndiye Katibu wa Organaizesheni katika Tawi.

Wakuu wa CCM wa Tawi

42. (1) Kutakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao katika Tawi:

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi

(b) Katibu wa CCM wa Tawi

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi.

Mwenyekiti wa CCM wa Tawi

43. (1) Mwenyekiti wa CCM wa Tawi atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi. Atakuwa katika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(2) Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya CCM katika Tawi.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Tawi, Mkutano wa Wanachama wote wa Tawi, Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Tawi na Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi.

(4) Katika Mikutano anayoiongoza, zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa CCM wa Tawi atakuwa pia na kura ya uamuzi, endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa kwamba kama Kikao anachokiongoza ni Kikao cha Uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za Wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

44. (1) Katibu wa CCM wa Tawi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi lake. Atakuwa katika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika. Katibu wa CCM wa Tawi

(2) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCM katika Tawi, na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri kuu ya CCM ya Tawi lake. majukumu yake ni haya yafuatayo:- .

(a) Kuratibu kazi zote za CCM katika Tawi.

(b) Kuitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Tawi kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Siasa ya Tawi na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(c) Kusimamia kazi za Utawala na Uendeshaji wa Chama katika Tawi.

(d) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na Maadili ya Chama katika Tawi.

(e) Kusimamia Udhibiti wa Fedha na Mali ya Chama katika Tawi.

(f) Kuitisha mikutano ya Kamati ya Siasa ya Tawi, Halmashauri Kuu ya Tawi na Mkutano Mkuu wa Tawi baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa CCM wa Tawi.

(3) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Tawi.

(4) Atashughulikia masuala yote ya Organaizesheni ya CCM katika Tawi, ambayo ni:-

(a) Masuala yote ya wanachama.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya vikao vya Chama.

(c) Kusimamia Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia masuala yote ya Uchaguzi wa ndani ya CCM ngazi ya Shina na Tawi, na ule wa Uwakilishi katika vyombo vya Dola,

(e) Kusimamia Muundo, Katiba, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

45. Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi na atashughulikia masuala yote ya Siasa na Uenezi katika Tawi. Majukumu yake ni haya yafuatayo:- Katibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi

(a) Kusimamia, kueneza na kufafanua masuala yote ya Itikadi, Siasa na Sera za CCM katika Tawi.

(b) Kushughulikia mafunzo na maandalizi ya Makada na Wanachama katika Tawi.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za kijamii na Ilani za uchaguzi za CCM katika Tawi.

(d) Kuwa na mipango ya mawasiliano na uhamasishaji wa Umma katika Tawi.

(e) Kufuatilia hali ya kisiasa na harakati za Vyama vya Siasa katika Tawi.

(f) Kufuatilia mwenendo wa Jumuiya za Kijamii katika Tawi.

Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi

46. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Tawi na atashughulikia masuala yote ya Uchumi na Fedha katika Tawi. Majukumu yake ni haya yafuatayo:

(a) Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi katika Tawi.

(b) Kubuni njia mbalimbali za kukipatia Chama mapato.

(c) Kutekeleza mipango ya uchumi na uwekezaji wa Chama katika Tawi.

(d) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Tawi.

(e) Kusimamia mali za Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Tawi.

## FUNGU LA III

## VIKAO VYA KATA/WADI

47. Kutakuwa na Vikao vya CCM vifuatavyo katika kila Kata ya Tanzania Bara yenye Matawi ya CCM yasiyopungua mawili, na katika kila Wadi ya Zanzibar:- Vikao vya CCM vya Kata/Wadi

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(3) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi.

(4) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

48. (1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi utakuwa na Wajumbe wafuatao:- Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/ Wadi.

(e) Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo linalohusika anayetokana na CCM anayeishi katika Kata/Wadi hiyo, au katika Kata/Wadi ambayo atakuwa ameichagua mwenyewe kwa madhumuni hayo.

(f) Wenyeviti wote wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(g) Makatibu wote wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(h) Makatibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(i) Makatibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(j) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Tawi kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi.

(k) Mjumbe mmoja anayewakilisha Tawi la CCM kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo na wa Wilaya.

(l) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(m) Wajumbe kumi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya na wajumbe watano wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Jimbo Zanzibar.

(n) Wajumbe waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, mmoja kutoka kila Kata ya Tanzania Bara na watano kutoka kila Wadi ya Zanzibar.

(o) Wenyeviti wote wa Serikali za Vijiji/Mitaa wa Kata/Wadi hiyo wanaotokana na CCM.

(p) Diwani wa Kata/Wadi anayetokana na CCM anayewakilisha Kata/Wadi hiyo, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Kata/Wadi hiyo.

(q) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya wanaoishi katika Kata/Wadi hiyo.

(r) Mwenyekiti na Katibu wa Kata/Wadi wa jumuiya inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM na mjumbe mmoja mwingine ambaye ni mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya inayohusika iliyomo katika Kata/Wadi hiyo.

(2) Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi ndicho kikao kikuu cha CCM katika Kata/Wadi.

(3) Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi utafanyika kwa kawaida mara moja kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo kutatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya kikao cha juu.

(4) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi ataongoza Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Mkutano huo utamchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

49. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi zitakuwa zifuatazo: Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi

(1) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za CCM katika Kata/Wadi iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi ya juu yanatekelezwa ipasavyo.

(3) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu Ulinzi na Usalama, na maendeleo kwa jumla katika Kata/Wadi.

(4) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Kuwachagua wajumbe watano wa kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(c) Kuwachagua wajumbe watano wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa upande wa

Zanzibar na wajumbe kumi wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(d) Kuwachagua wajumbe wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, mmoja kutoka kila Kata ya Tanzania Bara na watano kutoka kila Wadi ya Zanzibar.

(5) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/ Wadi

50. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi.

(e) Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo linalohusika anayetokana na CCM anayeishi katika Kata/Wadi hiyo, au katika Kata/Wadi ambayo atakuwa

ameichagua mwenyewe kwa madhumuni hayo.

(f) Diwani anayetokana na CCM anayewakilisha Kata/Wadi husika, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Kata/Wadi hiyo.

(g) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi hiyo.

(h) Wenyeviti wote wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(i) Makatibu wote wa CCM wa Matawi ya Kata/Wadi hiyo.

(j) Makatibu wote wa Siasa na Uenezi wa Matawi yaliyomo katika Kata/Wadi hiyo.

(k) Makatibu wote wa Uchumi na Fedha wa Matawi yaliyomo katika Kata/Wadi hiyo.

(l) Wenyeviti wote wa Serikali za vijiji/Mitaa wanaotokana na CCM katika Kata/Wadi hiyo.

(m) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya waliomo katika Kata/Wadi hiyo.

(n) Mwenyekiti na Katibu wa Kata/Wadi, na mjumbe mmoja mwingine ambaye ni mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya ya wananchi iliyomo katika Kata/Wadi hiyo.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itafanya Mikutano yake ya kawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu, lakini naweza kufanya mikutano isiyo ya kawaida wakati wowote endapo kutatokea haja ya kufanya hivyo.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi ataongoza Mkutano wa Halmshauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi; lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Kata/Wadi atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi

51. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea katika eneo lake la Kata/Wadi.

(2) Kusimamia uenezi wa Itikadi na Siasa ya CCM, na kueleza mipango ya CCM kwa Matawi yote ya Kata/Wadi na

kubuni mbinu zinazofaa za kuimarisha CCM katika eneo la Kata/Wadi inayohusika.

(3) Kupanga mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo.

(4) Kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusimamia utekelezaji wa siasa na maazimio ya CCM kwa jumla.

(5) Kuona kwamba unakuwepo Ulinzi na Usalama katika eneo la Kata/Wadi hiyo.

(6) Kuziongoza Halmashauri Kuu za CCM za Matawi yaliyomo katika Kata/Wadi hiyo kuhusu vitendo na njia zinazofaa za kuimarisha CCM.

(7) Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama pamoja na viongozi wa CCM na inapolazimu kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(8) Kufikisha Matawini maazimio na maagizo ya vikao vya juu na kufikisha kwenye Vikao vya juu mapendekezo kutoka Matawini.

(9) Unapofika wakati wa Uchaguzi Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Kumchagua Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi.

(c) Kumchagua Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi.

(d) Kuwachagua wajumbe watatu wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi kutoka miongoni mwao.

(e) Kwa Tanzania Bara itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba kugombea Uenyekiti wa Vitongoji vya Kata hiyo.

(f) Kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa Wanachama wanaoomba Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Tawi, Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi, Jimbo na Wilaya wanaotoka katika Tawi hilo.

(g) Kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanachama wa CCM watakaosimama katika uchaguzi

wa Mwenyekiti na Katibu wa Tawi wa kila Jumuiya inayoongozwa na CCM na wajumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Matawi yaliyomo katika Kata/Wadi hiyo

(10) Kujaza, kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi, nafasi za uongozi zinazokuwa wazi, isipokuwa ya Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(11) Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya CCM vilivyo chini yake.

(12) Kumsimamisha uanachama mwanachama yeyote wa ngazi ya Tawi au Shina ambaye mwenendo na tabia yake vinamuondolea sifa za uanachama.

(13) Kuunda Kamati Ndogo za Utekelezaji kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa kazi za CCM katika Kata/Wadi hiyo.

(14) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Ndogo za Utekelezaji wa kazi za CCM za Kata/Wadi na Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi.

(15) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM ya Kata/Wadi.

Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi

52. (1) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi.

(e) Diwani anayetokana na CCM anayewakilisha Kata/Wadi hiyo, na Madiwani wa aina nyingine wanaotokana na CCM wanaoishi katika Kata/wadi hiyo.

(f) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi hiyo.

(g) Mwenyekiti wa Kata/Wadi wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM katika Kata/Wadi hiyo.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itakutana si chini ya mara moja kila mwezi.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi ataongoza Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria Katibu wa CCM wa Kata/Wadi atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

53. Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi zitakuwa zifuatazo:- Kazi za Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika Kata/Wadi hiyo.

(2) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM katika Kata/Wadi hiyo.

(3) Kuandaa mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Kata/Wadi hiyo.

(4) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM katika Kata/Wadi chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi hiyo.

(5) Kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote wa ngazi ya Tawi au Shina endapo itaridhika kwamba tabia na

mwenendo wake vinamuondolea sifa ya uongozi.

(6) Kupanga mipango ya kukipatia Chama mapato, kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mipango hiyo, kudhibiti mapato na kusimamia matumizi bora ya fedha na mali za Chama katika Kata/Wadi.

(7) Unapofika wakati wa Uchaguzi Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itashughulikia mambo yafuatayo:

(a) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya uongozi wa CCM kupitia Kata/Wadi hiyo.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya juu ya wanachama wanaoomba Udiwani, Uenyekiti wa Mtaa, Ujumbe wa Kamati ya Mtaa, Uenyekiti wa Kijiji na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa mujibu wa sheria za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi juu ya Wanachama wa CCM wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa Tawi wa Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM, na Ujumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Kata/Wadi hiyo.

(8) Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(9) Kuona kwamba masuala wa Ulinzi na Usalama katika Kata/Wadi yanazingatiwa.

54. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi itakuwa na wajumbe wafuatao:- Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi

(a) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(b) Katibu wa Siasa na Uenezi Kata/Wadi.

(c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi,

(d) Makatibu wa Kata/Wadi wa Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM.

Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi

55. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kuongoza na kusimamia shughuli za Chama katika Kata/Wadi.

(b) Kuandaa Vikao vyote vya Chama vya Kata/Wadi.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(b) Idara ya Siasa na Uenezi ya Kata/Wadi.

(c) Idara ya Uchumi na Fedha ya Kata/Wadi.

(d) Idara ya Organaizesheni ya Kata/Wadi.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi isipokuwa kwamba Katibu wa CCM wa Kata/Wadi atakuwa ndiye Katibu wa Organaizesheni katika Kata/Wadi.

56. Kutakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao katika Kata/Wadi:- Wakuu wa CCM wa Kata/Wadi

(1) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi.

(2) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi.

(3) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi.

(4) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi.

57. (1) Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi. Atashika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika. Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi

(2) Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya CCM katika Kata/Wadi.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Kata/Wadi, Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi na Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(4) Katika mikutano anayoiongoza, zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa CCM wa Kata/Wadi pia

atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za Wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa kwamba kama kikao anachokiongoza ni kikao cha uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za Wajumbe zimelingana. Wajumbe wa Kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

Katibu wa CCM wa Kata/Wadi

58. (1) Katibu wa CCM wa Kata/Wadi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi.

(2) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCM katika Kata/Wadi na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi yake. Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuratibu kazi zote za CCM katika Kata/Wadi.

(b) Kuitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(c) Kusimamia kazi zote za Utawala na Uendeshaji wa Chama katika Kata/Wadi.

(d) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na maadili ya Chama katika Kata/Wadi.

(e) Kusimamia Udhibiti wa Fedha na Mali ya Chama katika Kata/Wadi.

(3) Ataitisha Mikutano ya Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi, Halmashauri Kuu ya Kata/Wadi na Mkutano Mkuu wa Kata/Wadi baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa CCM wa Kata Wadi.

(4) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Kata/Wadi.

(5) Atashughulikia masuala yote ya Organaizesheni ya CCM katika Kata/Wadi, ambayo ni:-

(a) Masuala yote ya wanachama.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya Vikao vya Chama.

(c) Kusimamia Jumuiya za wananchi zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia masuala yote ya Uchaguzi ndani ya Chama na ule wa uwakilishi katika vyombo vya Dola,

(e) Kusimamia Muundo, Katiba, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/ Wadi

59. Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi na atashughulikia masuala yote ya Siasa na Uenezi katika Kata/Wadi. Majukumu yake ni haya yafutayo:-

(a) Kusimamia, kueneza na kufafanua masuala yote ya Itikadi, Siasa na Sera za Chama katika Kata/Wadi.

(b) Kupanga na kusimamia mafunzo na maandalizi ya Makada na wanachama katika Kata/Wadi.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za Chama za Kijamii na Ilani za Uchaguzi za Chama katika Kata/Wadi.

(d) Kuwa na mipango ya Mawasiliano na Uhamasishaji wa Umma katika Kata/Wadi.

(e) Kufuatilia hali ya kisiasa na harakati za Vyama vya Siasa katika Kata/Wadi.

(f) Kufuatilia mwenendo wa Jumuiya za Kijamii katika Kata/Wadi.

60. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi na atashughulikia masuala yote ya Uchumi na Fedha katika Kata/Wadi. Majukumu yake ni haya yafuatayo:- Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/ Wadi

(a) Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi katika Kata/Wadi.

(b) Kutekeleza Sera za CCM za Uchumi na uwekezaji wa Chama katika Kata/Wadi.

(c) Kubuni njia mbalimbali za kukipatia Chama mapato.

(d) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi,

(e) Kusimamia mali za Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Kata/Wadi.

## FUNGU LA IV

## VIKAO VYA JIMBO

61. Kwa upande wa Zanzibar, kutakuwa na Vikao vya CCM vifuatavyo katika kila Jimbo:- *Vikao Vya CCM vya Jimbo*

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(3) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Jimbo.

(4) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

62. (1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo la Zanzibar utakuwa na wajumbe wafuatao:- *Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo Zanzibar*

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo.

(b) Katibu wa CCM wa Jimbo.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo.

(e) Mbunge au Mwakilishi anayetokana na CCM, na

wabunge au Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Jimbo hilo.

(f) Wenyeviti wote wa CCM wa Matawi ya Jimbo hilo.

(g) Makatibu wote wa CCM wa Matawi ya Jimbo hilo.

(h) Makatibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Matawi yote ya Jimbo hilo.

(i) Makatibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Matawi yote ya Jimbo hilo.

(j) Mwenyekiti na Katibu wa CCM wa kila Wadi ya Jimbo.

(k) Makatibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM wa Wadi zote za Jimbo.

(l) Makatibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Wadi zote za Jimbo.

(m) Wenyeviti na Makatibu wa Jumuiya za CCM wa Wadi zote za Jimbo.

(n) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(o) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Wadi iliyomo katika Jimbo hilo.

(p) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Jimbo wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(q) Wajumbe waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, watano kutoka kila Wadi ya Zanzibar.

(r) Madiwani wanaotokana na CCM wanaowakilisha Wadi zilizomo katika Jimbo husika, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Wadi zaJimbo hilo.

(s) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya na Mkoa waliomo katika Jimbo hilo.

(t) Mwenyekiti na Katibu wa Jimbo wa jumuiya inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM, na mjumbe mmoja mwingine ambaye ni mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya iliyomo katika Jimbo hilo.

(2) Mkutano Mkuu wa Jimbo ndicho kikao kikuu cha CCM katika Jimbo.

(3) Mkutano Mkuu wa Jimbo utafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa mwaka, lakini unaweza kufanyika wakati wowote mwingine endapo itatokea haja ya kufanya hivyo, au kwa maagizo ya vikao vya juu.

(4) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo ataongoza Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Mkutano utamchagua mjumbe mwingine ye yote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo

63. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za CCM katika Jimbo iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo na

kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi ya juu yanatekelezwa ipasavyo.

(3) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu Ulinzi na Usalama na maendeleo kwa jumla katika Jimbo.

(4) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo.

(b) Kuwachagua wajumbe watano wa kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(c) Kuwachagua wajumbe watano wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(d) Kuwachagua wajumbe watatu wa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa.

(5) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

64. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo.

(b) Katibu wa CCM wa Jimbo.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo.

(e) Mbunge na Mwakilishi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Jimbo husika, na Wabunge au Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Jimbo hilo.

(f) Madiwani wanaotokana na CCM wanaowakilisha Wadi zilizomo katika Jimbo husika, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Wadi za Jimbo hilo.

(g) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano wa Jimbo kuingia katika Halmashauri Kuu ya Jimbo.

(h) Wenyeviti wote wa CCM wa Wadi za Jimbo hilo.

(i) Makatibu wote wa CCM wa Wadi za Jimbo hilo.

(j) Makatibu wote wa Siasa na Uenezi wa Wadi za Jimbo hilo.

(k) Makatibu wote wa Uchumi na Fedha wa Wadi za Jimbo hilo.

(l) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ya CCM waliomo katika Jimbo hilo.

(m) Mwenyekiti na Katibu wa Jimbo wa Jumuiya inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM, na Mjumbe mmoja mwingine ambaye ni mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya inayohusika iliyomo katika Jimbo hilo.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo itafanya mikutano yake ya kawaida kila baada ya miezi mitatu, lakini inaweza kufanya mikutano isiyo ya kawaida wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo ataongoza Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Jimbo; lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Jimbo atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

65. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea katika eneo lake la Jimbo.

(2) Kusimamia uenezi wa Itikadi na Siasa ya CCM, na kueleza mipango ya CCM kwa Wadi zote za Jimbo, na kubuni mbinu zinazofaa za kuimarisha CCM katika eneo la Jimbo.

(3) Kupanga mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo.

(4) Kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusimamia utekelezaji wa Siasa na maazimio ya CCM kwa jumla katika Jimbo.

(5) Kuona kwamba unakuwepo Ulinzi na Usalama katika eneo la Jimbo.

(6) Kuziongoza Halmashauri Kuu za CCM za Wadi za Jimbo kuhusu vitendo na njia zinazofaa za kuimarisha CCM.

(7) Kuangalia mwenendo na vitendo vya Wanachama pamoja na Viongozi wa CCM waliomo katika Jimbo hilo, na inapolazimu, kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(8) Kufikisha kwenye Wadi maazimio na maagizo ya vikao vya juu na kufikisha kwenye Vikao vya juu mapendekezo kutoka Wadi.

(9) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Katibu wa CCM wa Jimbo.

(b) Kumchagua Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo.

(c) Kumchagua Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo.

(d) Kuwachagua Wajumbe watatu wa kamati Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo kutoka miongoni mwao.

(e) Kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanachama wa CCM watakaosimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti na Katibu wa Wadi wa kila Jumuiya inayoongozwa na CCM na wajumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Wadi zote za Jimbo hilo.

(10) Kujaza kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo nafasi za uongozi zinazokuwa wazi, isipokuwa ya Mwenyekiti wa Jimbo.

(11) Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya CCM vilivyo chini yake.

(12) Kuunda Kamati Ndogo za Utekelezaji kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa kazi za CCM katika Jimbo.

(13) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Ndogo za Utekelezaji wa Kazi za CCM za Jimbo na kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo.

(14) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM ya Jimbo.

66. (1) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo itakuwa na wajumbe wafuatao:- Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo.

(b) Katibu wa CCM wa Jimbo.

(c) Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Jimbo.

(d) Katibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Jimbo.

(e) Mbunge na Mwakilishi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Jimbo linalohusika na Wabunge au Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Jimbo hilo.

(f) Madiwani wanaotokana na CCM wanaowakilisha Wadi husika na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Wadi za Jimbo hilo

(g) Wajumbe watatu waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo hilo.

(h) Mwenyekiti wa Jimbo wa kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa na CCM katika Jimbo hilo.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Jimbo itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila baada ya miezi miwili.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo ataongoza Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Jimbo. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Jimbo atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

67. Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika Jimbo.

(2) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM Jimboni chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(3) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM katika Jimbo.

(4) Kuandaa mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Jimbo.

(5) Kupanga mipango ya kukipatia Chama mapato, kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mipango hiyo, kudhibiti

mapato na kusimamia matumizi bora ya fedha na mali za Chama katika Jimbo.

(6) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Kamati ya Siasa ya Jimbo itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake wa Kamati ya Siasa ya Wilaya juu ya wanachama wanaoomba nafasi za Uenyeketi na Ukatibu wa CCM wa Kata/Wadi, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi na Wanachama wanaoomba Uongozi wa CCM wa Jimbo kupitia Jimbo hilo.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Wilaya juu ya wanachama wanaoomba Udiwani au Uwakilishi wa aina nyingine katika Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Jimbo juu ya wanachama wa CCM wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa Wadi wa kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa na CCM; na ujumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Wadi.

(7) Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(8) Kuona kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama katika Jimbo yanazingatiwa.

Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

68. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Katibu wa CCM wa Jimbo ambaye atakuwa Mwenyekiti,

(b) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo,

(c) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo,

(d) Makatibu wa Jimbo wa Jumuiya za wananchi zinazoongozwa na CCM.

69. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo yatakuwa yafuatayo:-

Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo

(a) Kuongoza na kusimamia shughuli za Chama katika Jimbo.

(b) Kuandaa vikao vyote vya Chama vya Jimbo.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Jimbo yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu wa CCM wa Jimbo.

(b) Idara ya Siasa na Uenezi ya Jimbo.

(c) Idara ya Uchumi na Fedha ya Jimbo.

(d) Idara ya Organaizesheni ya Jimbo.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Jimbo isipokuwa kwamba Katibu wa CCM wa Jimbo atakuwa ndiye Katibu wa Organaizesheni katika Jimbo.

Wakuu wa CCM katika Jimbo

70. Kutakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao katika Jimbo:-

(1) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo.

(2) Katibu wa CCM wa Jimbo,

(3) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo,

(4) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo.

Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo

71. (1) Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo. Atashika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(2) Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya CCM katika Jimbo.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Jimbo, Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo na Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo.

(4) Katika mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo pia atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za Wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa

kwamba kama kikao anachokiongoza ni kikao cha uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

72. (1) Katibu wa CCM wa Jimbo atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo. Katibu wa CCM wa JImbo

(2) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCM katika Jimbo na atafanya kazi chini ya Halmashauri Kuu ya Jimbo lake.

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuratibu kazi zote za CCM katika Jimbo.

(b) Kuitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Jimbo kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Siasa ya Jimbo na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(c) Kusimamia kazi za Utawala na Uendeshaji wa Chama katika Jimbo.

(d) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na Maadili ya Chama katika Jimbo.

(e) Kusimamia Udhibiti wa fedha na mali ya Chama katika Jimbo.

(3) Ataitisha Mikutano ya Kamati ya Siasa ya Jimbo, Halmashauri Kuu ya Jimbo na Mkutano Mkuu wa Jimbo baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo

(4) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Jimbo.

(5) Atashughulikia na kusimamia masuala yote ya Organaizesheni ya CCM katika Jimbo, ambayo ni:-

(a) Masuala yote ya wanachama.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya vikao vya CCM.

(c) Kusimamia Jumuiya za wananchi zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia masuala yote ya Uchaguzi wa ndani ya Chama na ule wa Uwakilishi katika Vyombo vya Dola.

(e) Kusimamia Katiba, Muundo, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo

73. Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo na atashughulikia masuala yote ya Siasa na Uenezi katika Jimbo. Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kusimamia, kueneza na kufafanua masuala yote ya Itikadi, Siasa na Sera za CCM katika Jimbo.

(b) Kupanga na kusimamia Mafunzo na maandalizi ya Makada na Wanachama katika Jimbo.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za Chama za Kijamii na Ilani za Uchaguzi za CCM katika Jimbo.

(d) Kudumisha uhusiano mzuri na vyombo vya habari na kuwa na mipango ya mawasiliano na uhamasishaji wa Umma katika Jimbo.

(e) Kufuatilia hali ya kisiasa na harakati za Vyama vya Siasa Jimboni.

(f) Kufuatilia mwenendo wa Jumuiya za Kijamii katika Jimbo.

Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo

74. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo na atashughulikia masuala yote ya Uchumi na Fedha katika Jimbo. Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi katika Jimbo.

(b) Kutekeleza Sera za CCM za uchumi katika Jimbo.

(c) Kubuni na kutekeleza njia mbalimbali za kukipatia Chama mapato.

(d) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Jimbo.

(e) Kusimamia mali za Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Jimbo.

## FUNGU LA V

## VIKAO VYA WILAYA

75. Kutakuwa na Vikao vya CCM vifuatavyo katika kila Wilaya:- *Vikao vya CCM vya Wilaya*

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(2 Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(3) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(4) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(5) Kamati ya Madiwani wote wa CCM.

76. (1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya utakuwa na wajumbe wafuatao:- *Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya*

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(b) Katibu wa CCM wa Wilaya.

(c) Mkuu wa Wilaya ambaye anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya.

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

(f) Mbunge au Wabunge wanaotokana na CCM, wanaowakilisha Majimbo yaliyomo katika Wilaya hiyo, na Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(g) Wawakilishi wanaotokana na CCM, wanaowakilisha Majimbo yaliyomo katika Wilaya hiyo, na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo

(h) Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya hiyo.

(i) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(j) Mwenyekiti na Katibu wa Wilaya wa kila jumuiya ya wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM, na mjumbe mwingine mmoja ambaye ni mwanachama wa CCM aliyechaguliwa na kila Jumuiya inayohusika iliyomo katika Wilaya hiyo.

(k) Wajumbe wote ambao ni wanachama wa CCM kutoka

kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM wanaowakilisha Jumuiya hizo katika Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(m) Madiwani wanaotokana na CCM wanaowakilisha Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya husika na Madiwani wa CCM wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(n) Meya wa Manispaa au Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya anayetokana na CCM.

(o) Makatibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi za Wilaya hiyo.

(p) Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi za Wilaya hiyo.

(q) Wajumbe kumi waliochaguliwa na kila Kata ya Wilaya hiyo.

(r) Mjumbe mmoja aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Tawi la Wilaya hiyo.

(s) Wenyeviti wote wa CCM wa Matawi katika Wilaya hiyo.

(t) Makatibu wote wa CCM wa Matawi katika Wilaya hiyo.

(u) Makatibu wa Siasa na Uenezi wote wa Matawi ya CCM yaliyomo katika Wilaya hiyo.

(v) Makatibu wa Uchumi na Fedha wote wa Matawi yaliyomo katika Wilaya hiyo.

(w ) Wajumbe wengine wote wa Mkutano Mkuu wa Mkoa wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(x) Kwa Wilaya za Zanzibar, Wajumbe wengine wa Mkutano Mkuu wa Wilaya ni hawa wafuatao:-

- Wenyeviti na Makatibu wote wa CCM wa Majimbo.

- Makatibu wa Siasa na Uenezi wa Majimbo.

- Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Majimbo.

- Wenyeviti na Makatibu wa Majimbo wa Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

- Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya na Mkoa kupitia kila Jimbo linalohusika.

(2) Mkutano Mkuu wa Wilaya ndicho kikao kikuu cha CCM katika Wilaya.

(3) Madiwani wote wanaotokana na CCM kwa pamoja watakuwa Kamati ya Madiwani wa CCM ambayo kazi yake itakuwa ni kusimamia kwa jumla utekelezaji wa ilani ya CCM na siasa ya CCM katika shughuli zote zinazoendeshwa na Halmashauri za Wilaya, pamoja na kutekeleza kazi nyingine ambazo zimeainishwa katika kanuni zake zinazohusika. Vikao vya Kamati hii vitafanyika kwa mujibu wa Kanuni zake zinazohusika. Kwa upande wa Wilaya za Zanzibar, kwa kuwa Wilaya hizo zina Wabunge wengi pamoja na Wawakilishi wengi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi yaliyomo katika Wilaya husika, pamoja na Wabunge na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo, utaratibu utakuwa kwamba Wabunge wanaohusika

watachagua wajumbe wawili kutoka miongoni mwao; na Wawakilishi wanaohusika pia watachagua wajumbe wawili kutoka miongoni mwao, ambao ndio watakuwa Wajumbe wa Kamati ya Madiwani wote wa CCM katika Halmashauri inayohusika.

(4) Mkutano Mkuu wa Wilaya utafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila mwaka, lakini unaweza kukutana wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya vikao vya juu.

(5) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ataongoza Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya; lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria Mkutano utamchagua mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya

77. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za CCM iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya, na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.

(3) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu ulinzi na usalama na maendeleo kwa jumla katika Wilaya.

(4) Unapofika wakati wa uchaguzi Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya utashughulikia mambo yafuatayo:-

   (a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

   (b) Kuwachagua Wajumbe kumi kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

   (c) Kuwachagua Wajumbe wawili kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa.

   (d) Kuwachagua Wajumbe watano kuhudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa.

(5) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(6) Mkutano Mkuu wa Wilaya waweza kukasimu madaraka yake kwa Halmashauri Kuu ya Wilaya kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri utakavyoona inafaa.

Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

78. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(b) Katibu wa CCM wa Wilaya.

(c) Mkuu wa Wilaya ambaye anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya,

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

(f) Mbunge au Wabunge wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo yaliyomo katika Wilaya husika, na Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(g) Wawakilishi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Jimbo husika, na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(h) Wajumbe kumi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(i) Mwenyekiti, Katibu wa Wilaya na Mjumbe mmoja ambao ni wanachama CCM kutoka kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM iliyopo Wilayani wanaowakilisha Jumuiya hiyo kwenye Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya.

(j) Wenyeviti wa CCM wa Majimbo yaliyomo katika Wilaya hiyo.

(k) Makatibu wa CCM wa Majimbo yaliyomo katika Wilaya hiyo.

(l) Makatibu wa Siasa na uenezi wa Majimbo yaliyomo katika Wilaya hiyo.

(m) Makatibu wa uchumi na Fedha wa Majimbo yaliyomo katika wilaya hiyo

(n) Wenyeviti wa CCM wa Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya hiyo.

(o) Makatibu wa CCM wa Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya hiyo.

(p) Makatibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya hiyo.

(q) Makatibu wa CCM wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya hiyo.

(r) Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo anayetokana na CCM.

(s) Madiwani wanaotokana na CCM wanaowakilisha Kata/Wadi zilizomo katika Wilaya husika, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(t) Wajumbe wengine wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(u) Wajumbe wengine wa Halmashauri Kuu ya Wilaya wanaopatikana kwa mujibu wa kifungu 80 (9) (d).

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itafanya mikutano yake ya kawaida

mara moja kila baada ya miezi mitatu. Lakini inaweza kufanya mkutano usiokuwa wa kawaida wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

(3) Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Wilaya utakaofanyika katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya kila mwaka utakuwa pia na Kazi Maalum ya kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya CCM unaofanywa na mamlaka za Serikali za Mitaa katika Wilaya hiyo, katika mwaka wa Fedha uliopita wa mamlaka hizo, uliomalizika tarehe 31 Desemba ya mwaka unaohusika. Isipokuwa kwamba kwa Halmashauri ya Jiji, ambalo mipaka yake inaunganisha Wilaya zaidi ya moja, Taarifa zake zitapokelewa na kujadiliwa na Halmashauri Kuu ya Mkoa unaohusika na Mamlaka hiyo.

(4) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ataongoza Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya, lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Wilaya atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

79. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea katika eneo la Wilaya.

(2) Kusimamia Uenezi wa Itikadi na Siasa ya CCM na kueleza mipango ya CCM kwa Kata/Wadi na Majimbo yote ya Wilaya, na kubuni mbinu zinazofaa za kuimarisha CCM katika Wilaya.

(3) Kupanga mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Wilaya.

(4) Kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusimamia utekelezaji wa Siasa na Maazimio ya CCM kwa jumla.

(5) Kuona kwamba shughuli za maendeleo ya Ulinzi na Usalama zinazingatiwa katika Wilaya.

(6) Kuziongoza Halmashauri Kuu za CCM za Kata zote upande wa Tanzania Bara; na za Wadi na Majimbo upande wa Zanzibar, kuhusu njia zinazofaa za kuimarisha CCM na kuleta maendeleo Wilayani.

(7) Kuangalia mwenendo na vitendo vya wanachama pamoja na viongozi wa CCM katika Wilaya na inapolazimu kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(8) Kufikisha kwenye Kata, Wadi, Jimbo maazimio na maagizo ya vikao vya juu na kufikisha kwenye Vikao vya juu mapendekezo kutoka kwenye Kata/JWadi na Jimbo.

(9) Unapofika wakati wa uchaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kuwachagua kutoka miongoni mwao Wajumbe watano kwa Wilaya za Tanzana Bara, na watatu kwa Wilaya za Zanzibar kuingia katika Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya.

(b) Kumchagua Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM wa Wilaya.

(c) Kumchagua Katibu wa Uchumi na Fedha wa CCM wa Wilaya.

(d) Kuwachagua wanachama wasiozidi watatu wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(e) Kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa CCM wa Tawi, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi, Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi, Uenyekiti wa Mtaa,Ujumbe wa Kamati ya Mtaa, Uenyekiti na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(f) Kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanachama wa CCM watakaosimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti na Katibu wa Kata na Jimbo kwa upande wa Zanzibar wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM na Ujumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Kata na Majimbo katika Wilaya inayohusika.

(10) Kujaza kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya nafasi za Uongozi zinazokuwa wazi isipokuwa ya Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(11) Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya CCM vilivyo chini yake.

(12) Kuunda Kamati Ndogo za Utekelezaji kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa kazi za CCM katika Wilaya. Isipokuwa kwamba Halmashauri Kuu ya Wilaya itaunda Kamati Ndogo kwa kila Jimbo la Uchaguzi wa Wabunge/Wawakilishi lililomo katika Wilaya hiyo, ambayo itaitwa Kamati ya Jimbo. Kamati hiyo itakuwa na Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Wilaya wanaotoka katika Jimbo la Uchaguzi linalohusika, na itakuwa na uwezo wa kuchagua Mwenyekiti na Katibu wake. Kazi kubwa ya Kamati ya Jimbo la Uchaguzi itakuwa ni kubuni mbinu za kuimarisha Chama katika Jimbo hilo, pamoja na kupanga mikakati inayofaa ya Kampeni za uchaguzi kwa lengo la kuipatia CCM ushindi.

(13) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Kazi za CCM za Wilaya

na Kamati ya Madiwani wa CCM wa Wilaya.

(14) Kumwachisha au kumfukuza uongozi Mwenyekiti au Katibu wa CCM wa Tawi.

(15) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM ya Wilaya.

(16) Halmashauri Kuu ya Wilaya yaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati ya Siasa ya Wilaya kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri itakavyoona inafaa.

Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

80. (1) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(b) Katibu wa CCM wa Wilaya.

(c) Mkuu wa Wilaya ambaye anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya;

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

(f) Mbunge au Wabunge wanaotokana na CCM

wanaowakilisha Wilaya hiyo au Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo.

(g) Kwa Upande wa Wilaya za Zanzibar zenye Wabunge wengi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi yaliyomo katika Wilaya husika, na Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo, kwa pamoja watachagua wajumbe wasiozidi watano kutoka miongoni mwao, ambao ndio watakuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya inayohusika.

(h) Kwa upande wa Wilaya za Zanzibar zenye Wawakilishi wengi wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo ya uchaguzi yaliyomo katika Wilaya husika, pamoja na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Wilaya hiyo, kwa pamoja watachagua wajumbe wasiozidi watano kutoka miongoni mwao, ambao ndio watakuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya inayohusika.

(i) Wajumbe waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya kuingia katika Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya watano kwa Wilaya za Tanzania Bara na watatu kwa Wilaya za Tanzania Zanzibar.

(j) Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo anayetokana na CCM.

(k) Mwenyekiti wa Wilaya wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM iliyomo katika Wilaya hiyo.

(l) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Madiwani wa CCM.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kwa mwezi.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ataongoza Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria Katibu wa CCM wa Wilaya atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

81. Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya zitakuwa zifuatazo:-

Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika Wilaya.

(2) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM Wilayani chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(3) Kueneza Itikadi ya CCM katika Wilaya.

(4) Kuandaa mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo.

(5) Kupanga mipango ya kukipatia Chama mapato, kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mipango hiyo, kudhibiti mapato na kusimamia matumizi bora ya fedha na mali za Chama katika Wilaya.

(6) Unapofika wakati wa uchaguzi, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itashughulikia mambo yafuatayo:-

    (a) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa juu ya wanachama wanaoomba nafasi za uongozi wa CCM kupitia Wilaya hiyo.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya juu ya wanachama wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa CCM wa Tawi; Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Tawi, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Tawi; Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Kata/Wadi; Uenyekiti wa Mtaa, Uenyekiti na Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa juu ya Wanachama wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa CCM wa Jimbo; Katibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo; Katibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo; Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo, Wilaya na Mkoa, Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo, Uenyekiti na Ukatibu wa CCM wa Kata/Wadi, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata/Wadi; Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi na wagombea Udiwani wa CCM kwa mujibu wa sheria zilizopo za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

(d) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa, juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya na Mji, Meya na Naibu Meya wa Manispaa zilizomo katika Mkoa huo na wanachama wanaoomba nafasi za Ubunge na Uwakilishi.

(e) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Wilaya juu ya wanachama wa CCM wanaoomba Uenyekiti na Ukatibu wa Kata na Jimbo kwa upande wa Zanzibar wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM na wanaoomba Ujumbe wa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Kata na Majimbo katika Wilaya inayohusika.

(7) Kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote wa Kata/Wadi na Jimbo endapo itadhihirika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi.

(8) Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(9) Kuona kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama yanazingatiwa katika Wilaya.

Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

82. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(1) Katibu wa CCM wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(2) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya.

(3) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

(4) Makatibu wa Wilaya wa Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya

83. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kuongoza na kusimamia shughuli za Chama katika Wilaya.

(b) Kuandaa shughuli za vikao vyote vya Chama vya Wilaya.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu wa CCM wa Wilaya.

(b) Idara ya Siasa na Uenezi ya Wilaya.

(c) Idara ya Uchumi na Fedha ya Wilaya.

(d) Idara ya Organaizesheni ya Wilaya.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Wilaya isipokuwa kwamba Katibu wa CCM wa Wilaya atakuwa ndiye Katibu wa Organaizesheni katika Wilaya.

84. Kutakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao katika Wilaya:- Wakuu wa CCM katika Wilaya

(1) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(2) Katibu wa CCM wa Wilaya.

(3) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya.

(4) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

85. (1) Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya. Atashika nafasi hiyo kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika. Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya

(2) Atakuwa na wajibu wa kuangalia mambo yote ya CCM katika Wilaya.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya, Halmashauri Kuu

ya CCM ya Wilaya na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

(4) Katika mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya pia atakuwa na kura ya uamuzi endapo kura za wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa kwamba kama kikao anachokiongoza ni kikao cha Uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

Katibu wa CCM wa Wilaya

86. (1) Katibu wa CCM wa Wilaya atateuliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(2) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCM Wilayani na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya.

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuratibu kazi zote za CCM katika Wilaya.

(b) Kuitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Wilaya na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(c) Kusimamia kazi za Utawala na Uendeshaji wa Chama katika Wilaya,

d) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na Maadili ya Chama katika Wilaya.

(e) Kusimamia Udhibiti wa Fedha na Mali ya Chama Katika Wilaya.

(3) Kuitisha mikutano ya Kamati ya Siasa ya Wilaya, Halmashauri Kuu ya Wilaya na Mkutano Mkuu wa Wilaya baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya.

(4) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Wilaya.

(5) Atashughulikia na kusimamia masuala yote ya Organaizesheni ya CCM katika Wilaya, ambayo ni:-

(a) Masuala yote ya wanachama.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya vikao vya Chama.

(c) Kusimamia Jumuiya zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia masuala yote ya Uchaguzi wa ndani ya Chama na ule wa Uwakilishi katika Vyombo vya Dola.

(6) Kusimamia Katiba, Muundo, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya

87. Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya na atashughulikia masuala yote ya Siasa na Uenezi katika Wilaya. Majukumu yake ni haya yafuatayo:

(a) Kushughulikia masuala yote ya Itikadi, Siasa na Sera za CCM katika Wilaya,

(b) Kupanga na kusimamia Mafunzo na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Wilaya.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za Chama za Kijamii na Ilani za Uchaguzi za CCM katika Wilaya.

(d) Kudumisha uhusiano mzuri na Vyombo vya Habari na kuwa na mipango ya mawasiliano na uhamasishaji wa umma kwa ujumla katika Wilaya

(e) Kufuatilia hali ya Kisiasa na harakati za Vyama vya Siasa Wilayani.

(f) Kufuatilia mwenendo wa Jumuiya za kijamii katika Wilaya.

88. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya Wilaya na atashughulikia masuala yote ya Uchumi na Fedha katika Wilaya. Majukumu yake ni haya yafuatayo:- Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya

(a) Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa sera za CCM za Uchumi katika Wilaya,

(b) Kubuni na kufuatilia mipango ya Vitega Uchumi na Uwekezaji wa Chama katika ngazi ya Wilaya.

(c) Kutekeleza mipango ya vitega uchumi na uwekezaji wa Chama katika ngazi ya Wilaya.

(d) Kuchochea na kuratibu vitega uchumi na mipango ya uwekezaji wa Chama katika ngazi za chini za Wilaya inayohusika,

(e) Kutafuta na kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Wilaya.

(f) Kusimamia mali za Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Wilaya.

## FUNGU LA VI

## VIKAO VYA MKOA

89. Kutakuwa na Vikao vya CCM vifuatavyo katika kila Mkoa: *Vikao vya CCM vya Mkoa*

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(3) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(4) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

90. (1): Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa utakuwa na Wajumbe wafuatao:- *Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa*

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(b) Katibu wa CCM wa Mkoa.

(c) Mkuu wa Mkoa ambaye anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa

(f) Mjumbe au Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya

Taifa nafasi ya Mkoa na Wajumbe wengine wa Halmashauri Kuu ya Taifa wanaoishi katika Mkoa huo.

(g) Wabunge wote wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo yaliyomo katika Mkoa husika, na Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Mkoa huo.

(h) Wawakilishi wote wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo yaliyomo katika Mkoa husika, na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Mkoa huo.

(i) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(j) Mwenyekiti, Katibu, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Mkoa na Mjumbe mwingine mmoja aliyechaguliwa na kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM iliyomo Mkoani.

(k) Meya wa Jiji au Mji wenye hadhi ya Jiji.

(l) Wajumbe wawili waliochaguliwa kutoka kila Wilaya.

(m) Wenyeviti na Makatibu wote wa CCM wa Wilaya za Mkoa huo.

(n) Wakuu wote wa Wilaya ambao wanatokana na CCM katika Mkoa huo.

(o) Makatibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya za Mkoa huo.

(p) Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya za Mkoa huo.

(q) Wenyeviti wa Halmashauri za Miji, Meya wa Manispaa na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya katika Mkoa huo.

(r) Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa, wanaowakilisha kila Wilaya ya Mkoa huo.

(s) Wenyeviti na Makatibu wa CCM wa Majimbo ya Mkoa unaohusika, wa Zanzibar.

(t) Wenyeviti na Makatibu wa CCM wa Kata/Wadi zilizomo katika Mkoa huo.

(u) Makatibu wa Siasa na Uenezi; na Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Majimbo ya CCM ya Mkoa unaohusika wa Zanzibar.

(v) Madiwani wote wanaotokana na CCM wanaowakilisha Kata/Wadi zilizomo katika Mkoa husika, na Madiwani wa aina nyingine wanaoishi katika Mkoa huo.

(w) Makatibu wa Siasa na Uenezi; na Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Kata/Wadi zilizomo katika Mkoa huo.

(x) Mjumbe mmoja kutoka kila Kata kwa upande wa Tanzania Bara na Wajumbe watano kutoka kila Wadi kwa upande wa Zanzibar waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Kata/Wadi iliyomo katika Mkoa huo.

(y) Wajumbe watatu waliochaguliwa kutoka kila Jimbo la Mkoa unaohusika wa Zanzibar.

(z) Wajumbe wa Baraza Kuu la Tifa ambao ni wanachama wa CCM wa kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM iliyomo Mkoani

(2) Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa ndicho kikao kikuu cha CCM katika Mkoa.

(3) Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa utafanya mikutano yake ya kawaida mara tatu katika kipindi cha miaka mitano. Mikutano miwili itakuwa ya uchaguzi na mmoja wa kazi. Lakini mkutano usio wa kawaida unaweza kufanyika wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya kikao cha juu.

(4) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa ataongoza Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, lakini asipoweza kuhudhuria mkutano huo utamchagua Mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo.

(5) Madiwani wote wanaoishi katika Jiji au Mji wenye hadhi ya Jiji wanaotokana na CCM kwa pamoja watakuwa ni Kamati ya Madiwani wa CCM ya Mkoa katika Jiji au Mji unaohusika. Kazi yake itakuwa ni kusimamia kwa jumla utekelezaji wa Ilani ya CCM na Siasa ya CCM katika shughuli zote zinazoendeshwa na Halmashauri ya Jiji au Halmashauri ya Mji wenye hadhi ya Jiji, pamoja na kutekeleza kazi nyingine ambazo zimeainishwa katika kanuni zake zinazohusika. Vikao vya Kamati hii vitafanyika kwa mujibu wa Kanuni zake hizo.

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa

91. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za CCM iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Siasa ya CCM kwa kipindi kijacho.

(2) Kuhakikisha kwamba maazimio na maagizo ya ngazi za juu yanatekelezwa ipasavyo.

(3) Kuzungumzia mambo yote yanayohusu Ulinzi na Usalama, na maendeleo kwa jumla katika Mkoa huo.

(4) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kumchagua Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(b) Kumchagua Mjumbe mmoja kwa Mikoa ya Tanzania Bara na Wajumbe wanne kwa Mikoa ya Zanzibar wa kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa nafasi za Mkoa.

(c) Kuwachagua Wajumbe wawili kutoka kila Wilaya ya Tanzania

Bara na Wajumbe watano kutoka kila Wilaya ya Zanzibar kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(4) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(5) Mkutano Mkuu wa Mkoa waweza kukasimu madaraka yake kwa Halmashauri Kuu ya Mkoa kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri utakavyoona inafaa.

92. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:- Halmashauri Kuu ya CCM ya MKoa

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(b) Katibu wa CCM wa Mkoa.

(c) Mkuu wa Mkoa ambaye anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

(f) Mjumbe au Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, nafasi za Mkoa huo.

(g) Wenyeviti wote wa CCM wa Wilaya za Mkoa huo.

(h) Makatibu wa CCM wa Wilaya za Mkoa huo.

(i) Makatibu wa Siasa na Uenezi na Makatibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya za Mkoa huo.

(j) Wabunge wote wanaotokana na CCM wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi yaliyomo katika Mkoa husika, na Wabunge wa aina nyingine wanaoishi katika Mkoa huo.

(k) Wawakilishi wanaotokana na CCM wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi yaliyomo katika Mkoa husika, na Wawakilishi wa aina nyingine wanaoishi katika Mkoa huo.

(l) Meya wa Jiji au Meya wa Mji wenye hadhi ya Jiji anayetokana na CCM

(m) Wenyeviti wa Halmashauri za Miji, Meya wa Manispaa au Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya katika Mkoa huo wanaotokana na CCM.

(n) Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Mkoa wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, wawili kutoka kila Wilaya ya Tanzania Bara na watano kutoka kila Wilaya ya Zanzibar.

(o) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Madiwani wa CCM ya Mkoa wenye Jiji au Mji wenye hadhi ya Jiji.

(p) Mwenyekiti, Katibu wa Mkoa na Mjumbe au wajumbe ambao ni Wanachama wa CCM wa Baraza Kuu la Taifa wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa au inayojishirikisha na CCM iliyopo Mkoani.

(q) Wajumbe wengine wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa wanaopatikana kwa mujibu wa kifungu 94 (10) (d). (2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu, lakini inaweza kufanya mkutano usiokuwa wa kawaida wakati

wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya Kikao cha juu.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa ataongoza Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Mkoa atakuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa

93. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kuongoza na kusimamia ujenzi wa Ujamaa na Kujitegemea katika Mkoa.

(2) Kusimamia Uenezi wa Itikadi na Siasa ya CCM, kueleza Mipango ya CCM kwa Wilaya za CCM za Mkoa huo, na kubuni mbinu zinazofaa za kuimarisha CCM katika Mkoa.

(3) Kupanga mikakati ya Kampeni za Uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Mkoa.

(4) Kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusimamia utekelezaji wa Siasa na maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa.

(5) Kuona kwamba shughuli za Maendeleo na za Ulinzi na Usalama katika Mkoa zinazingatiwa.

(6) Kupokea, kuzingatia na kuamua juu ya mapendekezo ya vikao vya CCM vilivyo chini yake.

(7) Kuziongoza Halmashauri Kuu za CCM za Wilaya katika njia zinazofaa za kuimarisha CCM, na za kuleta maendeleo katika Mkoa.

(8) Kuangalia mwenendo na vitendo vya Wanachama na viongozi wa CCM katika Mkoa na inapolazimu kutoa taarifa kwa vikao vinavyohusika.

(9) Kufikisha maazimio na maagizo ya vikao vya juu kwa ngazi za chini yake, na kufikisha mapendekezo kutoka ngazi hizo kwa vikao vya juu.

(10) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kuwachagua Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa, watano kwa Mikoa ya Tanzania Bara, na watatu kwa Mikoa ya Zanzibar kutoka miongoni mwao.

(b) Kumchagua Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(c) Kumchagua Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

(d) Kuwachagua wanachama watatu wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(e) Kwa upande wa Tanzania Bara, itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba Uenyekiti wa CCM wa Kata, Ukatibu wa CCM wa Kata, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Kata, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Kata, Udiwani, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya, Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya na Mkoa, Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya, Mkoa, na Taifa.

(e) Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, itafikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wanaoomba

Uenyekiti wa CCM wa Wadi; Ukatibu wa CCM wa Wadi; Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Wadi; Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Wadi, Udiwani; Uenyekiti wa CCM na Ukatibu wa CCM wa Jimbo, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Jimbo; Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Jimbo; Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya, Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo, Wilaya na Mkoa, Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya, Mkoa na Taifa.

(f) Kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanachama wa CCM wanaogombea Uenyekiti wa Wilaya wa kila Jumuiya ya Wananchi inayo ongozwa na CCM; na majina ya kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Wilaya za Mkoa unaohusika.

(11) Kujaza kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa nafasi za uongozi zitakazokuwa wazi isipokuwa ya Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(12) Kuunda Kamati Ndogo kwa kadri itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora zaidi wa kazi za CCM katika Mkoa.

(13) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Ndogo za utekelezaji wa kazi za CCM za Mkoa na Kamati ya Madiwani wa CCM ya Mkoa pale panapohusika.

(14) Kumwachisha au kumfukuza Uanachama Mwanachama yeyote endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za Uanachama. Mwanachama anayeachishwa au kufukuzwa Uanachama anaweza kukata rufaa kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(15) Kumwachisha au kumfukuza uongozi kiongozi yeyote ambaye uteuzi wake wa mwisho unafanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(16) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM ya Mkoa.

(17) Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa yaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa kuhusu utekelezaji wa Kazi zake kwa kadri itakavyoona inafaa.

Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa

94. (1) Kutakuwa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa katika kila Mkoa ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(b) Katibu wa CCM wa Mkoa.

(c) Mkuu wa Mkoa ambaye ni anatokana na CCM.

(d) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(e) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

(f) Mjumbe au Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa nafasi za Mkoa huo.

(g) Mwenyekiti wa Mkoa wa kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa na CCM katika Mkoa huo.

(h) Wajumbe waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya Mkoa kuingia katika Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa, watano kwa mikoa ya Tanzania Bara na watatu kwa Mikoa ya Zanzibar.

(i) Meya wa Jiji ambalo mipaka yake inaunganisha zaidi ya Wilaya moja anayetokana na CCM.

(j) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Madiwani wote wa CCM wa Jiji au Mji wenye hadhi ya Jiji.

(2) Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila mwezi.

(3) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa ataongoza Mkutano wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Katibu wa CCM wa Mkoa atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa

95. Kazi za Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika Mkoa.

(2) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM katika Mkoa.

(3) Kuandaa mikakati ya kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo katika Mkoa.

(4) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM na maamuzi yote ya CCM chini ya Uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(5) Kupanga mipango ya kukipatia Chama mapato, kusimamia kwa dhati utekelezaji wa mipango hiyo, kudhibiti mapato na kusimamia matumizi bora ya fedha na mali za Chama katika Mkoa.

(6) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kwa upande wa Tanzania Bara, itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Kata, Diwani, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Kata, na Wilaya; Katibu wa Uchumi na Fedha wa Kata na Wilaya; Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya na Mkoa. Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya na Mkoa na Ujumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa

(b) Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya Mwenyekiti wa CCM wa Jimbo, Katibu wa CCM wa Jimbo, Mwenyekiti wa CCM wa Wadi, Katibu wa CCM wa Wadi, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wadi na Jimbo. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wadi, Diwani, Katibu wa Siasa na Uenezi wa Wilaya; Katibu wa Uchumi na Fedha wa Wilaya; Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Jimbo, Wilaya na Mkoa, na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya, Mkoa na Taifa.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya wanachama wanaoomba nafasi ya uongozi katika kila Wilaya na Mkoa wa Tanzania Bara ambao uteuzi wao wa mwisho hufanywa na vikao vya juu.

(d) Kufikiria na Kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za uongozi katika kila Wilaya na Mkoa wa Zanzibar ambao uteuzi wao wa mwisho hufanywa na vikao vya juu.

(e) Kwa upande wa Tanzania Bara, itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za Umeya wa Jiji na Ubunge.

(f) Kwa upande wa Zanzibar, itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za Umeya wa Jiji, au Manispaa yenye hadhi ya Jiji, Ubunge na Uwakilishi.

(g) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa juu ya Wanachama wa CCM wanaoomba nafasi za uongozi katika Jumuiya za Wananchi

zinazoongozwa na CCM, ngazi ya Wilaya, ambazo uteuzi wake wa mwisho hufanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa unaohusika. Vile vile itafikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu na Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa kuhusu Wanachama wa CCM wanaoomba nafasi za uongozi wa kila Jumuiya ya CCM ngazi ya Mkoa.

(h) Kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya wanachama wa CCM watakaogombea nafasi za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri za Wilaya, na Naibu Meya wa Halmashauri za Manispaa na Miji.

(7) Kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote wa ngazi ya Wilaya endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi, isipokuwa kwamba haitakuwa na uwezo wa kumsimamisha uongozi Kiongozi ambaye uteuzi wake wa mwisho haukufanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(8) Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(9) Kuona kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama na ya Maendeleo yanazingatiwa katika Mkoa.

96. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:- *Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa*

(1) Katibu wa CCM wa Mkoa ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(2) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(3) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

(4) Makatibu wa Mkoa wa Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM.

97. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa yatakuwa yafuatayo:- *Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa*

(a) Kuongoza na kusimamia shughuli za Chama katika Mkoa.

(b) Kuandaa shughuli za vikao vyote vya Chama vya Mkoa.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Mkoa yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu wa CCM wa Mkoa

(b) Idara ya Siasa na Uenezi ya Mkoa.

(c) Idara ya Uchumi na Fedha ya Mkoa.

(d) Idara ya Organaizesheni ya Mkoa.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa isipokuwa kwamba Katibu wa CCM wa Mkoa atakuwa ndiye Katibu wa Organaizesheni katika Mkoa.

Wakuu wa CCM wa Mkoa

98. Kutakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao katika Mkoa:-

(1) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(2) Katibu wa CCM wa Mkoa.

(3) Mjumbe au Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa nafasi ya Mkoa.

(4) Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa.

(5) Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa

99. (1) Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa na atashika nafasi hiyo ya Uongozi kwa muda wa miaka

mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(2) Atakuwa na madaraka ya kuangalia mambo yote ya CCM katika Mkoa.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa, Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa.

(4) Katika Mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa atakuwa pia na kura ya uamuzi iwapo kura za wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa kwamba kama kikao anachokiongoza ni kikao cha Uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo kura za wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

100. (1) Katibu wa CCM wa Mkoa atateuliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Katibu wa CCM wa Mkoa

(2) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za CCM katika Mkoa na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri

Kuu ya CCM ya Mkoa wake. Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuratibu kazi zote za CCM katika Mkoa.

(b) Kuitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati ya Siasa ya Mkoa na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(c) Kusimamia kazi za Utawala na Uendeshaji wa Chama katika Mkoa.

(d) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na Maadili ya Chama katika Mkoa.

(e) Kusimamia Udhibiti wa Fedha na Mali ya Chama katika Mkoa.

(3) Ataitisha Mikutano ya Kamati ya Siasa ya Mkoa, Halmashauri Kuu ya Mkoa na Mkutano Mkuu wa Mkoa baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa.

(4) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi katika Mkoa

(5) Atashughulikia na kusimamia masuala yote ya Organaizesheni ya CCM katika Mkoa, ambayo ni:-

(a) Masuala yote ya wanachama.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya vikao vya Chama.

(c) Kusimamia Jumuiya zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia na kuratibu masuala yote ya Uchaguzi wa ndani ya Chama na ule wa Uwakilishi katika vyombo vya Dola.

(e) Kusimamia Katiba, Muundo, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

101. Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na atashughulikia masuala yote ya Siasa na Uenezi katika Mkoa. Majukumu yake ni haya yafuatayo:- Katibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa

(a) Kusimamia, kueneza na kufafanua masuala yote ya Itikadi, Siasa na Sera za CCM katika Mkoa.

(b) Kupanga na kusimamia Mafunzo na Maandalizi ya Makada na Wanachama katika Mkoa.

(c) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za Chama za Kijamii na Ilani za Uchaguzi za CCM katika Mkoa.

(d) Kudumisha uhusiano mzuri na Vyombo vya Habari na kuwa na mipango ya mawasiliano na Uhamasishaji wa Umma kwa jumla katika Mkoa.

(e) Kufuatilia hali ya Kisiasa Mkoani.

(f) Kufuatilia mwenendo wa Jumuiya za Kijamii Mkoani

Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa

102. Katibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na atashughulikia masuala yote ya Uchumi na Fedha katika Mkoa. Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha na kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi katika Mkoa.

(b) Kubuni na kufuatilia mipango ya Vitega Uchumi na Uwekezaji wa Chama ngazi ya Mkoa.

(c) Kuchochea na kuratibu vitega uchumi na mipango ya uwekezaji wa Chama katika Wilaya zote za Mkoa.

(d) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa.

(e) Kusimamia mali ya Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa.

KATIBA YA CCM:Layout 1  6/5/10  11:59 AM  Page 156

## FUNGU LA VII

## VIKAO VYA TAIFA

103. Kutakuwa na Vikao vifuatavyo vya CCM vya Taifa:- Vikao vya CCM vya Taifa

(1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa.

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(3) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (Zanzibar).

(5) Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

(6) Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(7) Kamati ya Wabunge wote wa CCM.

(8) Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wa CCM (Zanzibar).

104. (1) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:- Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa

(a) Mwenyekiti wa CCM.

(b) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaotokana na CCM.

(c) Makamu wawili wa Mwenyekiti wa CCM.

(d) Rais wa Zanzibar anayetokana na CCM.

(e) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanaotokana na CCM.

(f) Katibu Mkuu wa CCM

(g) Manaibu Katibu Mkuu wa CCM.

(h) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni.

(i) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi.

(j) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(k) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

(l) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(m) Wabunge wote wanaotokana na CCM au kama Bunge limevunjwa wale wanachama wote waliokuwa Wabunge mara kabla ya kuvunjwa Bunge; na Wabunge wote wa Bunge la Afrika Mashariki wanaotokana na CCM.

(n) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaotokana na CCM au kama Baraza hilo limevunjwa wale wanachama wote waliokuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mara kabla ya kuvunjwa kwa Baraza hilo.

(o) Makatibu wa Siasa na Uenezi wote wa Mikoa.

(p) Makatibu wa Uchumi na Fedha wote wa Mikoa

(q) Wenyeviti wote wa CCM wa Wilaya.

(r) Makatibu wote wa CCM wa Wilaya.

(s) Makatibu wote wa Siasa na Uenezi wa Wilaya.

(t) Makatibu wote wa Uchumi na Fedha wa Wilaya.

(u) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM.

(v) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaotokana na CCM.

(w) Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Makamu Mwenyekiti wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM ambao ni wanachama wa CCM.

(x) Wajumbe watano waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa kila Wilaya.

(y) Wajumbe watano waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kila wilaya ya CCM ya Vyuo vya Elimu ya Juu nchini.

(z) Mwenyekiti, Katibu wa Mkoa na Mjumbe mwingine mmoja aliyechaguliwa kutoka kila Mkoa wa Bara na Zanzibar kwa kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa au iliyojishirikisha na CCM ambao ni wanachama wa CCM.

(2) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utakuwa ndicho Kikao Kikuu cha CCM kupita vyote na ndicho kitakachokuwa na madaraka ya mwisho.

(3) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utafanya mikutano yake ya kawaida

mara tatu katika kipindi cha miaka mitano. Mikutano miwili kati ya hiyo itakuwa ya uchaguzi na mmoja utakuwa wa kazi. Kalenda ya vikao vya Chama itaonyesha ni lini mikutano hiyo mitatu itafanyika. Lakini mkutano usiokuwa wa kawaida unaweza kufanyika wakati wowote ukiitishwa na Mwenyekiti wa CCM au ukiombwa na theluthi mbili ya wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Taarifa ya kukutana Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa ni lazima itolewe si chini ya miezi mitatu kabla ya tarehe ya kukutana. Lakini inaweza kutolewa taarifa ya muda mfupi zaidi ya huo ikiwa unafanyika mkutano usiokuwa wa kawaida.

(5) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa unaweza kukiagiza kikao chochote cha CCM kufanya kazi zozote ambazo ni za Mkutano huo bila Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa wenyewe kuathiri uwezo wake wa kufanya kazi hizo.

(6) Wabunge wote wanaotokana na CCM kwa pamoja watakuwa ni Kamati ya Wabunge wa CCM ambao kazi yake itakuwa ni kusimamia kwa jumla

utekelezaji wa Ilani ya CCM na Siasa ya CCM katika shughuli zote zinazoendeshwa na Bunge, pamoja na kutekeleza kazi nyingine ambazo zimeainishwa katika Kanuni zake zinazohusika. Vikao vya Kamati hii vitafanyika kwa mujibu wa Kanuni zake hizo.

(7) Kamati hii itakuwa na uwezo wa kutunga Kanuni zake kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli zake. Kanuni hizo itabidi ziidhinishwe na Halmashauri Kuu ya Taifa kabla hazijaanza kutumika.

(8) Mwenyekiti wa CCM anaweza kuamua kuitisha vikao vya pamoja baina ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na Kamati ya Wabunge wote wa CCM kwa ajili ya kushughulikia mambo kama itakavyoonekana inafaa.

(9) Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM pamoja na Katibu wa Kamati hiyo watakuwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(10) Unapofika wakati wa uchaguzi, Kamati ya Wabunge wote wa CCM itachagua Wajumbe kumi (10) kutoka miongoni

mwao, kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

(11) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaotokana na CCM kwa pamoja watakuwa ni Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM ambayo kazi yake itakuwa ni kusimamia kwa jumla utekelezaji wa Ilani ya CCM na Siasa ya CCM katika shughuli zote zinazoendeshwa na Baraza la Wawakilishi, pamoja na kutekeleza kazi nyingine ambazo zimeainishwa katika Kanuni zake zinazohusika. Vikao vya Kamati hii vitafanyika kwa mujibu wa Kanuni zake hizo.

(12) Kamati hii itakuwa na uwezo wa kutunga Kanuni zake kwa ajili ya uendeshaji bora wa shughuli zake na kwamba Kanuni hizo itabidi ziidhinishwe na Halmashauri Kuu ya Taifa kabla ya kuanza kutumika.

(13) Mwenyekiti wa CCM anaweza kuitisha vikao vya pamoja baina ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM kwa ajili ya kushughulikia mambo kama itakavyoonekana inafaa.

(14) Mwenyekiti wa Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM pamoja na Katibu wa Kamati hiyo watakuwa Wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(15) Unapofika wakati wa uchaguzi, Kamati ya Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaotokana na CCM watachagua Wajumbe watano (5) kutoka miongoni mwao kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

(16) Kiwango cha mahudhurio ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kitakuwa ni theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Zanzibar.

(17) Mwenyekiti wa CCM atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa na asipoweza kuhudhuria, mmoja wa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM ataongoza Mkutano huo. Iwapo itatokea kwamba wote watatu hawawezi kuhudhuria Mkutano fulani, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itamchagua Mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo kwa ajili ya shughuli hiyo. Kutokana na hali hiyo Halmashauri Kuu ya CCM ya

Taifa inaweza kukutana hata kama Mwenyekiti na Makamu wote wawili wa Mwenyekiti hawapo.

105. Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa zitakuwa zifuatazo:-

Kazi za Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa

(1) Kupanga Siasa ya CCM na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za CCM.

(2) Kupokea na kufikiria taarifa ya kazi za CCM iliyotolewa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa na kutoa maelekezo ya mipango na utekelezaji wa Siasa ya CCM Kwa kipindi kijacho.

(3) Kuthibitisha, kubadili, kukataa au kuvunja uamuzi wowote uliotolewa na kikao chochote cha chini yake au na yeyote wa CCM.

(4) Kubadili sehemu yoyote ya Katiba ya CCM kwa uamuzi wa theluthi mbili za Wajumbe walio na haki ya kupiga kura kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar.

(5) Unapofika wakati wa uchaguzi, Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa utashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kuwachagua Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM.

(b) Kuchagua jina moja la Mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Kuchagua jumla ya Wajumbe themanini na tano kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wa kuingia katika Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kutoka orodha ya Taifa.

(6) Kuunda Kamati za Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(7) Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa waweza kukasimu madaraka yake kwa Halmashauri Kuu ya Taifa kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri itakavyoona inafaa.

Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

106. (1) Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa CCM.

(b) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaotokana na CCM.

(c) Makamu wawili wa Mwenyekiti wa CCM.

(d) Rais wa Zanzibar anayetokana na CCM.

(e) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanaotokana na CCM.

(f) Katibu Mkuu wa CCM

(g) Manaibu Katibu Mkuu wa CCM.

(h) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni.

(i) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi.

(j) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(k) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

(l) Wenyeviti wote wa CCM wa Mikoa.

(m) Makatibu wote wa CCM wa Mikoa.

(n) Mwenyekiti, Katibu Mkuu na Makamu Mwenyekiti kutoka kila Jumuiya ya wananchi inayoongozwa au inayojishirikisha na CCM.

(o) Wajumbe wengine wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa wanaopatikana kwa mujibu wa vifungu: 92(4)(b); 105(10); 105(15); 106(5)(c) na 108(13)(e).

(p) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM

(q) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM.

(r) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayetokana na CCM na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar anayetokana na CCM.

(s) Wajumbe wa Heshima wasiozidi watano walioteuliwa na Mwenyekiti wa CCM kuingia Kamati Kuu, kutokana na uongozi wao uliotukuka

(2) Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila baada ya miezi minne,

lakini inaweza kufanya mkutano usiokuwa wa kawaida wakati wowote endapo itatokea haja ya kufanya hivyo au kwa maagizo ya kikao cha juu. Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa utakaofanyika katika kipindi cha miezi sita ya mwisho wa kila mwaka utakuwa pia na kazi maalum ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM unaofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mwaka wa fedha uliopita wa Serikali hizo ambao ulimalizika tarehe 30 Juni ya mwaka unaohusika.

(3) Katika mikutano yote ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, uamuzi utafikiwa kwa makubaliano ya jumla, au kwa wingi wa kura za Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura. Lakini ukitokea uamuzi unaohitajika kutolewa kuhusu vyombo vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kuhusu muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, uamuzi huo ni lazima upitishwe kwa azimio lililoungwa mkono na theluthi mbili ya kura za Wajumbe kutoka

Tanzania Bara na theluthi mbili ya kura za Wajumbe kutoka Zanzibar.

(4) Mwenyekiti wa CCM atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, lakini Mwenyekiti wa CCM asipoweza kuhudhuria, mmoja wa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

107. Kazi za Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa zitakuwa zifuatazo:-

(1) Kutoa uongozi wa Siasa ya CCM kwa jumla kwa Tanzania nzima. Kwa hiyo itakuwa na uwezo wa kubuni, kujadili, kuamua na kutoa Miongozo ya Siasa ya CCM katika mambo mbalimbali.

(2) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM, kuongoza mafunzo ya Siasa ya CCM na kukuza nadharia na Itikadi ya CCM ya Ujamaa na Kujitegemea.

(3) Kuongoza na kusimamia ujezi wa Ujamaa na Kujitegemea nchini.

(4) Kuandaa Ilani ya CCM ya Uchaguzi na kutoa msukumo wa utekelezaji wa Ilani hiyo.

(5) Kufikisha maazimio na maagizo ya CCM katika Mikoa na kufikiria na kutoa uamuzi juu ya mapendekezo kutoka vikao vya CCM vya chini.

(6) Kuona kwamba shughuli za Maendeleo na za Ulinzi na Usalama wa Taifa zinazingatiwa.

(7) Kuandaa mikakati na mbinu za kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo za kitaifa.

(8) Kudumisha uangalizi juu ya vitendo vya Wanachama na Viongozi wa CCM na endapo itadhihirika kwamba tabia na mwenendo wa Mwanachama fulani vinamwondolea sifa za Uanachama au Uongozi itakuwa na uwezo wa kumwachisha au kumfukuza Uanachama au Uongozi alio nao. Kuhusu mtu aliyeachishwa au kufukuzwa Uanachama, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa ndiyo itakayokuwa na uwezo wa mwisho wa kumrudishia Uanachama wake kwa mujibu wa Katiba, endapo itaridhika kuwa amejirekebisha.

(9) Kuziongoza Halmashauri Kuu za CCM za Mikoa kuhusu vitendo na njia zinazofaa za kuimarisha CCM na za kuleta maendeleo.

(10) Kuandaa Katiba, Kanuni na kuweka taratibu za kuongoza shughuli mbalimbali za CCM.

(11) Kuandaa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa

(12) Kuteua Makatibu wa CCM wa Mikoa.

(13) Unapofika wakati wa Uchaguzi, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kuteua jina la Mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa CCM, na majina mawili ya Wanachama watakaosimama katika uchaguzi wa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM.

(b) Kupendekeza kwa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa majina yasiyozidi matatu ya Wanachama wanaogombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuyawasilisha mbele ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa.

(c) Kuchagua jina moja la Mwanachama atakayesimama katika uchaguzi wa Rais wa Zanzibar.

(d) Kuwachagua Katibu Mkuu wa CCM, Manaibu Katibu Mkuu wa CCM, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

(e) Kuwachagua Wanachama wasiozidi kumi kuwa Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kutokana na mapendekezo ya Mwenyekiti wa CCM.

(f) Kuwachagua Wajumbe kumi na wanne wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa kutoka miongoni mwao, wakiwemo wanawake wasiopungua wanne, wawili kutoka Tanzania Bara na wawili kutoka Zanzibar.

(g) Kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya Wanachama wanaoomba nafasi ya Ubunge na majina ya Wanachama wanaoomba

nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa sheria zilizopo za uchaguzi huo.

(h) Kufikiria na kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya Wanachama wanaoomba nafasi ya Ujumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa; Uenyekiti wa CCM wa Wilaya na Mikoa, Ukatibu wa Siasa na Uenezi wa Mkoa, Ukatibu wa Uchumi na Fedha wa Mkoa.

(i) Kufanya uteuzi wa mwisho wa majina ya Wanachama wa CCM wanaogombea Uenyekiti wa Mkoa, Uenyekiti wa Taifa na Ukatibu Mkuu wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM, na majina ya Wanachama watakaochaguliwa kuiwakilisha kila Jumuiya katika vikao vya CCM vya Mkoa na Taifa.

(j) Kuwachagua jumla ya Wajumbe wanane wa Baraza la Wadhamini kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

(14) Kujaza kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa, nafasi za uongozi

zitakazokuwa wazi, isipokuwa ya Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM.

(15) Kuunda Kamati au Tume kwa shughuli maalum bila kuathiri majukumu ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(16) Kupokea na kujadili taarifa za Tume na Kamati Maalum za CCM, Kamati ya Wabunge wa CCM, na Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM.

(17) Kuweka kiwango cha kiingilio katika CCM, ada za Uanachama na michango maalum.

(18) Kusimamisha kwa maslahi ya CCM utumiaji wa kifungu chochote cha Katiba ya CCM au kuruhusu kifungu kutumika kabla ya kuingizwa ndani ya Katiba. Uamuzi huo sharti uungwe mkono na theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Zanzibar. Hata hivyo Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafikisha uamuzi wake mbele ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(19) Kushughulikia uhusiano kati ya CCM na Jumuiya mbalimbali za wananchi na kuziorodhesha Jumuiya zinazoongozwa au zinazojishirikisha na CCM.

(20) Kutengeneza na kurekebisha Muundo wa CCM katika maeneo na nyanja mbalimbali kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(21) Kumsimamisha Mwenyekiti wa CCM au Makamu Mwenyekiti wa CCM iwapo mwenendo na utendaji wake wa kazi vinamwondolea sifa za uongozi. Hata hivyo Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafikisha mapendekezo yake mbele ya Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(22) Kumwachisha au kumfukuza Uongozi kiongozi yeyote ambaye uteuzi wake wa mwisho ulifanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(23) Kuunda Kamati ya Usalama na Maadili.

(24) Kuidhinisha Kanuni za Kamati za Wabunge wote wa CCM, Wawakilishi wote wa CCM, Madiwani wote wa CCM; Katiba/Kanuni za Jumuiya za wananchi zinazoongozwa na CCM na kuidhinisha marekebisho ya Katiba/Kanuni hizo.

(25) Halmashauri Kuu ya Taifa yaweza kukasimu madaraka yake kwa Kamati Kuu kuhusu utekelezaji wa kazi zake kwa kadri itakavyoona inafaa.

108. (1) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

(a) Mwenyekiti wa CCM.

(b) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaotokana na CCM.

(c) Makamu wawili wa Mwenyekiti wa CCM.

(d) Rais wa Zanzibar anayetokana na CCM.

(e) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanaotokana na CCM.

(f) Katibu Mkuu wa CCM

(g) Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa CCM.

(h) Rais Mstaafu wa Zanzibar ambaye pia alikuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM.

(i) Manaibu Katibu Mkuu wa CCM.

(j) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizasheni.

(k) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi.

(l) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(m) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

(n) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano anayetokan a na CCM, na Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar anayetokana na CCM.

(o) Wajumbe wengine wasiozidi kumi na wanne waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa wakiwemo wanawake wasiopungua wanne, wawili kutoka Tanzania Bara na wawili kutoka Zanzibar.

(p) Mwenyekiti wa Taifa wa kila Jumuiya ya Wananchi inayoongozwa na CCM.

(q) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM.

(r) Mwenyekiti na Katibu wa Kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM.

(t) Wajumbe wengine wa Heshima wasiozidi watano watakaopendekezwa na Mwenyekiti wa CCM kutokana na uongozi wao uliotukuka.

(2) Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila miezi miwili.

(3) Mwenyekiti wa CCM atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, lakini Mwenyekiti wa CCM asipoweza kuhudhuria, mmoja wa Makamu wa Mwenyekiti atakuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

109. Kazi za Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa zitakuwa zifuatazo:

Kazi za Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

(1) Kutoa uongozi wa Siasa katika nchi.

(2) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM.

(3) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM nchini.

(4) Kusimamia kampeni za Uchaguzi na kampeni nyinginezo.

(5) Kuteua Makatibu wa CCM wa Wilaya, Katibu wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, Makatibu Wasaidizi Wakuu wa Idara na Wakuu wa Vitengo vya Makao Makuu ya Chama.

(6) Unapofika wakati wa Uchaguzi Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kufikiria na kutoa mapendekezo kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya Wanachama watakaosimama katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa CCM.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu majina ya Wanachama wasiozidi watano

wanaoomba kugombea kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya Wanachama watakaosimama katika uchaguzi wa Makamu wa Mwenyekiti wa CCM.

(d) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya majina ya Wanachama wasiozidi watatu ambao wanaomba kugombea kiti cha Rais wa Zanzibar.

(e) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za uongozi katika CCM na Jumuiya zinazoongozwa na CCM ambao uteuzi wao wa mwisho unafanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(f) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya

Wanachama wanaoomba nafasi ya Ubunge na Wanachama wanaoomba nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(g) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Halmashauri Kuu ya Taifa juu ya Wanachama wa CCM wanaoomba nafasi za uongozi katika Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM, ngazi ya Mkoa na Taifa, ambazo uteuzi wake wa mwisho hufanywa na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

(h) Kufikiria na Kufanya uteuzi wa mwisho wa wanachama wa CCM wanaoomba kugombea nafasi ya Spika wa Bunge/Baraza la Wawakilishi, Meya wa Halmashauri ya Jiji/Manispaa.

(7) Kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote isipokuwa Mwenyekiti wa CCM na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi.

(8) Kuona kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama wa Taifa na Maendeleo yanazingatiwa.

(9) Kuandaa mikutano ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(10) Kuwa na mikakati endelevu ya kuimarisha Chama kimapato, kudhibiti mapato na mali za Chama na kuthibitisha matumizi ya Chama katika ngazi ya Taifa.

Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

110. Kutakuwa na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(1) Katibu Mkuu wa CCM ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(2) Manaibu Katibu Mkuu wa CCM.

(3) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni.

(4) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi.

(5) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(6) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

(7) Makatibu Wakuu wa Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM.

Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

111. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kusimamia shughuli zote za utendaji za Chama kitaifa.

(b) Kuandaa shughuli za vikao vya Chama ngazi ya Taifa.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Katibu Mkuu wa CCM.

(b) Idara ya Organaizesheni.

(c) Idara ya Itikadi na Uenezi.

(d) Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(e) Idara ya Uchumi na Fedha.

(3) Kila Idara itaongozwa na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Idara ya Utawala na Uendeshaji Bara

au Zanzibar itaongozwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM.

(4) Kila Idara ya Makao Makuu ya Chama itakuwa na Kamati ya Ushauri yenye Wajumbe wasiozidi watano akiwemo na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Wajumbe hao watateuliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

112. Kazi za Idara za Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa:-

Kazi za Idara za Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa

(1) Idara ya Organaizesheni:-

(a) Kushughulikia masuala yote ya wanachama wa CCM.

(b) Kufuatilia vikao na maamuzi ya vikao vya Chama.

(c) Kusimamia Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM na Wazee wa Chama.

(d) Kusimamia masuala yote ya Uchaguzi wa ndani ya CCM na ule wa Uwakilishi katika Vyombo vya Dola.

(e) Kusimamia Katiba, Muundo, Kanuni na Taratibu za Chama na Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

(2) Idara ya Itikadi na Uenezi:-

(a) Kushughulikia masuala ya msingi ya Itikadi na Sera za Chama Cha Mapinduzi.

(b) Kueneza na kufafanua Itikadi na Sera za CCM.

(c) Kupanga na kusimamia Mafunzo na Maandalizi ya Makada na Wanachama.

(d) Kusimamia Vyombo vya Habari vya Chama, Mawasiliano na Uhamasishaji wa Umma kwa jumla

(e) Kuongoza na kusimamia maandalizi ya Sera, Programu na Ilani za Uchaguzi za CCM.

(f) Kusimamia Utafiti, Maktaba na Nyaraka za Chama.

(3) Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa:-

(a) Kufuatilia hali ya kisiasa nchini.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na Sera za Kijamii za CCM.

(c) Kufuatilia harakati za Vyama vya Siasa nchini.

(d) Kufuatilia maendeleo ya Jumuiya za Kijamii nchini.

(e) Kuratibu uhusiano na ushirikiano wa CCM na vyama vya siasa vya kidugu, kirafiki na vya kimapinduzi.

(f) Kufuatilia hali ya kisiasa katika nchi jirani na nchi nyinginezo duniani.

(g) Kufuatilia maendeleo ya Kamati za Urafiki na mshikamano kati ya Watanzania na wananchi wa nchi rafiki.

(h) Kushughulikia masuala ya Itifaki ndani ya Chama.

(4) Idara ya Uchumi na Fedha:-

(a) Kufuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi.

(b) Kuratibu mapato ya fedha za Chama nchini kote kwa ajili ya maamuzi ya uwekezaji wa Chama.

(c) Kusimamia vitega uchumi na uwekezaji katika Chama.

(d) Kusimamia Mali za Chama nchini kote.

(e) Kusimamia mapato na matumizi ya Chama katika ngazi zote za uongozi wa CCM.

Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar

113. (1) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar.

(b) Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar.

(c) Rais wa Zanzibar anayetokana na CCM.

(d) Waziri Kiongozi wa Zanzibar anayetokana na CCM.

(e) Wajumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kutoka Zanzibar.

(f) Wenyeviti wa CCM wa Mikoa ya Zanzibar.

(g) Makatibu wa CCM wa Mikoa ya Zanzibar.

(h) Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa wanaotoka Zanzibar.

(2) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itafanya mikutano yake ya kawaida mara moja kila miezi miwili.

(3) Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa atakuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM kutoka Zanzibar. Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa atakuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM kutoka Zanzibar.

(4) Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa ataongoza mikutano ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa. Lakini Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria, Mkutano huo utamchagua Mjumbe mwingine yeyote miongoni mwao kuwa Mwenyekiti wa muda wa mkutano huo.

114. Kazi za Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa zitakuwa zifuatazo:-

Kazi za Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar

(1) Kusaidia Kamati Kuu kutoa Uongozi wa Siasa Zanzibar.

(2) Kueneza Itikadi na Siasa ya CCM Zanzibar.

(3) Kuisaidia Kamati Kuu katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za CCM Zanzibar.

(4) Kutafuta na kubuni njia au mbinu mbalimbali zinazoweza kukifanya Chama kujitegemea kimapato Zanzibar.

(5) Kuandaa mikakati na mbinu za kampeni za uchaguzi na kampeni nyinginezo.

(6) Kuona kwamba masuala ya Ulinzi na Usalama na ya Maendeleo yanazingatiwa.

(7) Unapofika wakati wa Uchaguzi Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itashughulikia mambo yafuatayo:-

(a) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa juu ya Wanachama wanaoomba nafasi za uongozi katika CCM kutoka Zanzibar, ambao uteuzi wao wa mwisho unafanywa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(b) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu ya

Halmashauri Kuu ya Taifa juu ya Wanachama wanaoomba nafasi ya Rais wa Zanzibar, Ubunge na Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(c) Kupendekeza kwa Kamati Kuu kumsimamisha uongozi kiongozi yeyote wa CCM wa Zanzibar isipokuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM endapo itaridhika kwamba tabia na mwenendo wake vinamwondolea sifa za uongozi.

(d) Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa inaweza kuunda Kamati Ndogo za CCM. Aidha, inaweza kujiwekea utaratibu wake wa kufanya kazi kwa kadri itakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanikisha shughuli za CCM Zanzibar.

(e) Kuwachagua Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni Zanzibar, Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi Zanzibar, Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya

Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa Zanzibar na Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha, Zanzibar, kutoka miongoni mwao.

(f) Kupokea na kujadili taarifa za Kamati Ndogo za CCM.

(g) Kufikiria na kutoa mapendekezo yake kwa Kamati Kuu juu ya Wanachama wa CCM wanaoomba nafasi za uongozi katika Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM, ngazi ya Mkoa na Taifa kwa upande wa Zanzibar, ambazo uteuzi wake wa mwisho hufanywa na Halmashauri Kuu ya Taifa.

Sekretarieti ya Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar

115. Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(1) Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Zanzibar) ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(2) Katibu wa Kamati Maalum wa Idara ya Organaizesheni.

(3) Katibu wa Kamati Maalum wa Idara ya Itikadi na Uenezi.

(4) Katibu wa Kamati Maalum wa Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(5) Katibu wa Kamati Malum wa Uchumi na Fedha.

(6) Manaibu Katibu Mkuu wa Jumuiya za Wananchi zinazoongozwa na CCM wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar.

116. (1) Majukumu ya Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa yatakuwa yafuatayo:- Majukumu ya Sekretarieti ya Kamati Maalumu

(a) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za utendaji za Chama Zanzibar.

(b) Kuandaa shughuli za vikao vya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar.

(2) Majukumu ya Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa Zanzibar yatagawanyika ifuatavyo:-

(a) Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Zanzibar).

(b) Idara ya Organaizesheni, Zanzibar.

(c) Idara ya Itikadi na Uenezi, Zanzibar

(d) Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Zanzibar.

(e) Idara ya Uchumi na Fedha, Zanzibar.

(3) Kila Idara ya Zanzibar itaongozwa na Katibu wa Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa ambaye atateuliwa na Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Idara za Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa zitatekeleza kazi na majukumu ambayo kwa upande wa Bara yanatekelezwa na Idara za Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

Wakuu wa CCM

117. Chama cha Mapinduzi kitakuwa na Wakuu wa CCM wafuatao:-

(1) Mwenyekiti wa CCM.

(2) Makamu wawili wa Mwenyekiti wa CCM.

(3) Katibu Mkuu wa CCM.

118. Mwenyekiti wa CCM ndiye kiongozi mkuu na ndiye msemaji mkuu wa CCM. Mwenyekiti wa CCM

(1) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa na atakuwa katika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(2) Anaweza kuondolewa katika uongozi kwa azimio litakalopitishwa katika Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa na kuungwa mkono na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Zanzibar.

(3) Atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Katika mikutano anayoiongoza zaidi ya kuwa na kura yake ya kawaida Mwenyekiti atakuwa pia na kura ya uamuzi endapo kura za Wajumbe wanaoafiki na wasioafiki zitalingana. Isipokuwa kwamba kama kikao anachokiongoza ni kikao cha Uchaguzi, Mwenyekiti atakuwa na kura yake ya kawaida tu. Hatakuwa na haki ya kutumia kura yake ya uamuzi endapo

kura za wajumbe zimelingana. Wajumbe wa kikao wataendelea kupiga kura mpaka hapo mshindi atakapopatikana.

Makamu wa Mwenyekiti wa CCM

119. (1) Kutakuwa na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM wawili watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa. Kutakuwa na Makamu wa Mwenyekiti anayeishi na kufanyia kazi zake Tanzania Bara; na kutakuwa na Makamu wa Mwenyekiti wa CCM anayeishi na kufanyia kazi zake Zanzibar. Isipokuwa kwamba kuishi kwao hivyo hakutapunguza upeo wa madaraka yao ya kushughulikia kazi za CCM kwa Tanzania nzima.

(2) Makamu Mwenyekiti wa CCM atakuwa katika madaraka hayo kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(3) Makamu wa Mwenyekiti wa CCM anaweza kuondolewa katika madaraka hayo kwa azimio litakalopitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa na kuungwa mkono na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Tanzania Bara, na theluthi mbili za Wajumbe kutoka Zanzibar.

(4) Makamu wa Mwenyekiti watakuwa ndiyo wasaidizi wakuu wa Mwenyekiti wa CCM na watafanya kazi zote za CCM watakazopewa na Mwenyekiti wa CCM.

120. (1) Katibu Mkuu wa CCM atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa. Katibu Mkuu wa CCM

(2) Atakuwa Katibu wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(3) Atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa CCM na atafanya kazi chini ya uongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(4) Atakuwa na wajibu wa kuitisha Mikutano yote ya Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa na Mkutano Mkuu wa CCM wa Taifa.

(5) Ataitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa kwa madhumuni ya kushauriana, kuandaa agenda za Kamati Kuu, na kuchukua hatua za utekelezaji wa maamuzi ya CCM.

(6) Atakuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama nchini.

(7) Kazi na majukumu ya Katibu Mkuu wa CCM:-

(a) Kuratibu kazi zote za Chama Cha Mapinduzi.

(b) Kusimamia kazi za Utawala na Uendeshaji katika Chama.

(c) Kufuatilia na kuratibu masuala ya Usalama na Maadili katika Chama.

(d) Kusimamia Udhibiti wa Fedha na Mali za Chama.

Viongozi wengine wa Kitaifa wa CCM

121. Kutakuwa na Viongozi wengine wa CCM wa Kitaifa wafuatao:-

(1) Naibu Katibu Mkuu Bara na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar.

(2) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni.

(3) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi.

(4) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

(5) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha.

122. (1) Kutakuwa na Manaibu Katibu Mkuu wa CCM wawili. Manaibu Katibu Mkuu wa CCM

(2) Kutakuwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM atakayeishi na kufanyia kazi zake Tanzania Bara, na kutakuwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM atakayeishi na kufanyia kazi zake Zanzibar. Isipokuwa kwamba kuishi kwao hivyo hakutapunguza upeo wa madaraka yao ya kushughulikia kazi za CCM kwa Tanzania nzima.

(3) Naibu Katibu Mkuu wa CCM atakayefanya kazi Zanzibar atakuwa na wajibu wa kuandaa na kuitisha mikutano ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar, na ataitisha na kuongoza vikao vya Sekretarieti ya Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa Zanzibar.

(4) Manaibu Katibu Mkuu wa CCM watakuwa ndio wasaidizi wakuu wa Katibu Mkuu wa CCM na watafanya kazi zozote za CCM watakazopangiwa na Katibu Mkuu wa CCM.

123. (1) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa. Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Organaizesheni

(2) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa Organaizesheni ya CCM.

(3) Atakuwa Naibu Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama nchini na atafanya kazi hii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa CCM ambaye ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi

124. (1) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Itikadi na Uenezi atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(2) Atashughulikia masuala ya msingi ya Itikadi na Sera za CCM.

(3) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa shughuli za Uenezi wa Itikadi, Siasa na Sera za CCM.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa

125. (1) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(2) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa ndani ya Chama.

(3) Atashughulikia masuala ya kuimarisha uhusiano mwema baina ya CCM na vyama vya siasa vya nchi nyingine; na

harakati za vyama vya siasa na maendeleo ya Jumuiya za Kijamii nchini.

126. (1) Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha atachaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa. Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa wa Uchumi na Fedha

(2) Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa masuala ya Uchumi, Fedha na Mali za Chama.

(3) Atafuatilia utekelezaji wa Sera za CCM za Uchumi na ataratibu mapato ya fedha za Chama nchini kote kwa ajili ya maamuzi ya uwekezaji wa Chama.

KATIBA YA CCM:Layout 1  6/5/10  11:59 AM  Page 202

## SEHEMU YA NNE

## WAZEE NA JUMUIYA ZA WANANCHI

127. Kutakuwa na Sehemu ya Wazee ambamo watakuwemo Wazee wote wanaokubali imani, malengo, na madhumuni ya CCM. *Sehemu ya Wazee*

128. Chama Cha Mapinduzi kitakuwa na uhusiano na Jumuiya mbalimbali za Wananchi:- *Jumuiya za Wananchi*

(1) Kutakuwa na Jumuiya zinazoongozwa na CCM ambazo kwa sasa ni:-

(a) Umoja wa Vijana wa CCM **(UVCCM),**

(b) Umoja wa Wanawake Tanzania **(UWT).**

(c) Umoja wa Wazazi **(WAZAZI).**

(2) Kutakuwa na Jumuiya nyingine zilizojishirikisha na CCM.

(3) Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa inaweza kuongeza na kupunguza katika orodha, Jumuiya zinazoongozwa au zilizojishirikisha na CCM.

(4) Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa itakuwa na uwezo wa kushauri, kutoa

maagizo ya jumla, na maelekezo maalum kwa Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

(5) Halmashauri Kuu ya Taifa itathibitisha Kanuni/Katiba ya kila Jumuiya inayoongozwa na CCM na marekebisho yake kabla hazijatumika.

## SEHEMU YA TANO

## MENGINEYO

129. (1) Kutakuwa na Baraza la Wadhamini wa CCM. Baraza la Wadhamini wa CCM

(2) Baraza hilo litakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Mwenyekiti wa CCM kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza.

(b) Wajumbe wanane waliochaguliwa na Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa.

(c) Wenyeviti wa Mabaraza ya Wadhamini ya Jumuiya zinazoongozwa na CCM.

(3) Baraza la Wadhamini la CCM litafanya Vikao vyake kila baada ya miezi minne, yaani si chini ya mara tatu kwa mwaka.

(4) Baraza hili litakuwa na uwezo wote ule wa wadhamini kwa mujibu wa Sheria.

(5) Mali yote ya CCM inayoondosheka na isiyoondosheka, itakuwa mikononi mwa Baraza la Wadhamini.

(6) Kazi za Baraza hilo zitakuwa zifuatazo;

(a) Kusimamia Mali zote za Chama zinazoondosheka na zisizoondosheka

(b) Kufanya tathmini ya mara kwa mara ya mali za Chama.

(c) Kutoa ushauri juu ya mabadiliko yoyote yanayohitajika katika umiliki wa mali za Chama, kwa mfano kuhusu mali zinazostahili kuuzwa.

(d) Kutekeleza majukumu mengine yoyote ambayo yatakabidhiwa kwake na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

(7) Baraza hili litafanya kazi chini ya uongozi wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa na litawajibika kutoa taarifa yake kwa kikao hicho.

(8) Mdhamini atashika nafasi hiyo ya uongozi kwa muda wa miaka mitano, lakini anaweza kuchaguliwa tena baada ya muda huo kumalizika.

(9) Iwapo Mwenyekiti wa Baraza hili hataweza kuhudhuria Mkutano

wowote, Baraza lenyewe litachagua Mjumbe mwingine miongoni mwao atakayekuwa Mwenyekiti wa muda wa Mkutano huo.

130. Isipokuwa kama imeagizwa vingine katika Katiba hii ya CCM, kiwango cha mahudhurio katika mikutano ya CCM kitakuwa ni zaidi ya nusu ya Wajumbe walio na haki ya kuhudhuria katika kikao kinachohusika.

Kiwango cha Mahudhurio katika kufikia Uamuzi

131. Isipokuwa kama imeagizwa vingine katika Katiba hii ya CCM uamuzi utafikiwa katika vikao vyote vya CCM kwa kufuata makubaliano ya jumla au wingi wa kura za Wajumbe waliohudhuria na kupiga kura. Lakini katika shughuli zozote za uchaguzi wa Viongozi, kura zitakuwa za Siri.

Kiwango cha Kura katika kufikia Uamuzi

132. Wakati wowote kunapotokea nafasi wazi miongoni mwa viti vyovyote vya CCM, kikao kinachohusika kitajaza nafasi hiyo bila kuchelewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

Nafasi zikiwa wazi

133. (1) Mwanachama anayetaka kujiuzulu atafanya hivyo kwa kuandika barua ya kujiuzulu kwake na kuipeleka kwa Katibu wa Tawi lake.

Kujiuzulu

(2) Kiongozi anayetaka kujiuzulu atafanya hivyo kwa kuandika barua ya kujiuzulu kwake na kuipeleka kwa Katibu wa Kikao kilichomchagua au kumteua.

Kung'atuka

134\. (1) Kiongozi anayetaka kung'atuka atafanya hivyo kwa kuandika barua ya kung'atuka kwake na kuipeleka kwa Katibu wa kikao kilichomchagua au kumteua, au

(2) Kwa kutangaza uamuzi wa kung'atuka kwake mbele ya kikao kilichomchagua.

Kuacha Ujumbe wa Kikao

135\. Mjumbe yeyote wa kikao chochote kilichowekwa na Katiba hii ataacha kuwa Mjumbe wa kikao hicho iwapo hatahudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kikao chake isipokuwa kama ni kwa sababu zinazokubaliwa na kikao chenyewe.

## NYONGEZA "A"

## AHADI ZA WANACHAMA WA CHAMA CHA MAPINDUZI

(1) Binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja

(2) Nitaitumikia nchi yangu na watu wake wote.

(3) Nitajitolea nafsi yangu kuondosha umaskini, ujinga, magonjwa na dhuluma.

(4) Rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa.

(5) Cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu.

(6) Nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na kuitumia elimu yangu kwa faida ya wote.

(7) Nitashirikiana na wenzangu wote kujenga nchi yetu.

(8) Nitasema kweli daima, fitina kwangu mwiko.

(9) Nitakuwa mwanachama mwaminifu wa CCM na raia mwema wa Tanzania na Afrika.

## NYONGEZA "B"

Katiba, Kanuni na Taratibu za utekelezaji zilizotungwa katika kuongoza shughuli mbalimbali za CCM ni hizi zifuatazo:-

(1) Taratibu za Sehemu ya Wazee.

(2) Kanuni za Uchaguzi wa CCM.

(3) Kanuni za Utendaji kazi za Uongozi katika Chama Cha Mapinduzi.

(4) Kanuni za Fedha na Mali za Chama.

(5) Kanuni za Umoja wa Vijana wa CCM.

(6) Katiba ya Umoja wa Wanawake wa Tanzania.

(7) Kanuni za Umoja wa Wazazi.

(8) Kanuni za Uongozi na Maadili.

(9) Kanuni za Uteuzi wa Wagombea Uongozi katika Vyombo vya Dola.

(10) Kanuni za Kamati ya Wabunge wote wa CCM

(11) Kanuni za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wa CCM.

(12) Kanuni za Madiwani wote wa CCM.

(13) Kanuni za Utumishi wa Chama Cha Mapinduzi.

KATIBA YA CCM:Layout 1  6/5/10  11:59 AM  Page 211

KATIBA YA CCM:Layout 1 6/5/10 11:59 AM Page 212

**Imetolewa na Makao Makuu ya CCM,**
**S.L.P. 50, DODOMA**